



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

-----

**MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA  
BAJETI KWA MWAKA 2018/19**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO  
NOVEMBA, 2017**



## UTANGULIZI

1. Mwongozo wa Mpango na Bajeti umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti Na.11 ya Mwaka 2015 na Kanuni zake. Mwongozo wa Mwaka 2018/19 ni wa tatu katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Maandalizi ya Mpango na Bajeti yamezingatia: Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 ya Chama Tawala, Mpango wa Pili wa Maendeleo na Maelekezo ya Serikali.
2. Lengo kuu la Mwongozo wa Mpango na Bajeti ni kuelekeza namna bora ya ukusanyaji wa mapato na utengaji wa raslimali fedha za kutekeleza Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2018/19 ili kufikia mafanikio ya kijamii na kiuchumi na kupunguza umaskini nchini. Hivyo, Mwongozo wa Mpango na Bajeti unawaelekeza Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na mashirika ya Umma kuandaa mipango yao na bajeti kwa kuzingatia Sheria za Nchi, Kanuni, Nyaraka na Miongozo ya Serikali.
3. Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/19 umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inaelekeza namna ya kuandaa mpango na bajeti ili kupata matokeo yanayotarajiwa kwa mwaka 2018/19. Sehemu ya pili inabainisha hali ya uchumi na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2016/17 na mwenendo wa uchumi kwa robo ya kwanza ya mwaka 2017/18 pamoja na maoteo ya awali ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali. Sehemu zote mbili zinasomwa kwa pamoja ambapo, maoteo kwa mwaka 2018/19 yanapaswa kuzingatia masuala yanayoelekezwa katika sehemu ya kwanza. Aidha, Mwongozo huu unasomwa kwa pamoja na kiambatisho chake chenye majedwali mahususi yatakayotumiwa katika utayarishaji na uwasilishaji wa mpango na bajeti, utekelezaji na utoaji wa taarifa.
4. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia ufanisi wa matumizi ya fedha za umma, kwa kutenga fedha kwenye maeneo ya kimkakati ambayo utekelezaji wake utaleta matokeo makubwa katika kufikia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo na viashiria vya utekelezaji kwa mwaka 2018/19. Miongoni mwa maeneo hayo ni: kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali; kuimarisha sekta ya madini ikiwemo kuboresha usimamizi wa kodi; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ambapo pamoja na mambo mengine utahusisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, uimarishaji wa viwanja vya ndege, na kuimarisha mtandao wa barabara; kuimarisha kilimo ikiwemo miundombinu ya umwagiliaji; kuimarisha sekta ya mifugo na uvuvi; kuimarisha huduma za afya, elimu na maji safi na

salama; kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii nchini ikiwemo ujenzi wa miundombinu wezeshi; na kuboresha na kuimarisha shuguli za viwanda nchini.

## **SEHEMU I**

# **MAELEKEZO YA UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI**



## YALIYOMO

UTANGULIZI.....	iii
SEHEMU I .....	v
MAELEKEZO YA UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI .....	v
1.0 MABORESHO YA MIFUMO .....	1
2.0 UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI.....	3
3.0 MFUMO WA MAPATO NA MATUMIZI .....	6
4.0 MAMBO MENGINE YA KUZINGATIWA KATIKA UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI .....	12
5.0 MAELEKEZO MAHSUSI KWA SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.....	17
6.0 UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI .....	20
7.0 HITIMISHO.....	21
SEHEMU II .....	23
MAPITIO NA MWELEKEO WA BAJETI.....	23
SURA YA KWANZA .....	25
MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA UCHUMI .....	25
1.1 Usuli .....	25
1.2 Mwenendo wa Viashiria vya Uchumi.....	26
1.2.1 Viashiria vya Ndani vya Uchumi .....	26
1.2.2 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki .....	27
1.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti 2016/17.....	29
1.3.1 Mapato ya Ndani .....	29
1.3.2 Misaada na Mikopo Nafuu kutoka Nje.....	32
1.3.3 Matumizi.....	33
1.3.4 Deni la Taifa .....	34
1.4 Ujazi wa Fedha na Karadha.....	35
1.4.1 Ujazi wa Fedha.....	35
1.4.2 Mzunguko wa Sarafu .....	37
1.4.3 Mwenendo wa Viwango vya Riba na Udhibiti wa Ukwasi .....	38
1.4.4 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji Fedha .....	39

1.4.5	Mwenendo wa Sekta ya Benki.....	39
1.5	Mwenendo wa Sekta ya Nje .....	40
1.6	Mwelekeo wa Uchumi na Maoteo ya Muda wa Kati .....	42
1.6.1	Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia.....	42
SURA YA PILI .....		48
MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2018/19 - 2020/21 .....		48
2.1	Utangulizi .....	48
2.2	Sera za Kibajeti .....	49
2.2.1	Sera za Mapato .....	49
2.2.2	Sera za Matumizi .....	51
2.2.3	Usimamizi wa Malimbikizo ya Madeni.....	52
2.2.4	Sera za Kugharamia Nakisi ya Bajeti.....	53
2.3	Vigezo vya Ugawaji Rasilimali fedha katika Kipindi cha Muda wa Kati .....	57
2.3.1	Matumizi ya Kawaida .....	57
2.3.1.1	Vigezo Mahsusni kwa Sekretarieti za Mikoa .....	58
2.3.1.2	Vigezo Mahsusni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.....	59
2.3.2	Matumizi ya Maendeleo.....	60
KIAMBATISHO:MIUNDO YA UANDAAJI, UTEKELEZAJI NA UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI.....		61



## ORODHA YA VIFUPISHO

ADP	Annual Development Plan
AGOA	Africa Growth and Opportunity Act
AIDS	Acquired Immune Deficiency Syndrome
ARV	Antiretroviral
ATCL	Air Tanzania Company Limited
ATM	Average Time to Maturity
ATR	Average Time to Re-fixing
BRN	Big Results Now
CDR	Council Development Reporting
CFR	Council Financial Reporting
CFS	Consolidated Fund Services
CHF	Community Health Fund
CNHI	China Merchant Holding International
DART	Dar es Salaam Rapid Transit
DCF	Development Cooperation Framework
DPs	Development Partners
DRC	Democratic Republic of Congo
DSA	Debt Sustainability Analysis
DSF	Debt Sustainability Framework
DUCE	Dar es Salaam University College of Education
EAC	East Africa Community
EFD	Electronic Fiscal Devices
ENCB	External Non Concessional Borrowing
EPZ	Export Processing Zone
EPZ	Economic Processing Zone
EU	European Union
FEWSNET	Famine Early Warning System Network
FYDP	Five Year Development Plan
GBP	Great Britain Pound
GBS	General Budget Support
GDP	Gross Domestic Product
GNI	Gross National Income
GWh	Giga Watts Hour
HIPC	Highly Indebted Poor Countries
HIV	Human Immunodeficiency Virus
ICT	Information Communication Technology
IFMS	Integrated Financial Management Systems
IMF	International Monetary Fund
JAST	Joint Assistance Strategy for Tanzania

JNIA	Julius Nyerere International Airport
KIA	Kilimanjaro International Airport
KPIs	Key Performance Indicators
LGAs	Local Government Authorities
LGDG	Local Government Development Grant
LICs	Low Income Countries
LTPP	Long Term Perspective Plan
M3	Extended Broad Money Supply
MDAs	Ministries, Independent Departments and Agencies
MDGs	Millennium Development Goals
MDRI	Multilateral Debt Relief Initiatives
MEST	Ministry of Education, Science and Technology
MKUKUTA	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini
MoFP	Ministry of Finance and Planning
MSCL	Marine Service Company Limited
MTEF	Medium Term Expenditure Framework
MUCE	Mkwawa University College of Education
MW	Mega Watts
NDC	National Development Corporation
NDS	National Debt Strategy
NER	Net Enrolment Rate
NFA	Net Foreign Assets
NHIF	National Health Insurance Fund
NKRAs	National Key Results Areas
NOP	Net Open Position
OC	Other Charges
ODA	Official Development Assistance
OFC	Optic Fibre Cable
OPEC	Organisation of Petroleum Exporting Countries
OTR	Office of the Treasury Registrar
PBB	Program Based Budget
PC	Planning Commission
PE	Personnel Emoluments
PIM-OM	Public Investment Management - Operational Manual
PMO	Prime Ministers' Office
PO-	President Office, Public Service Management and Good
PSMGG	Governance
PO-RALG	Presidents' Office - Regional Administration and Local Government
PPP	Public Private Partnership
PV	Present Value
RSs	Regional Secretariats'
SADC	Southern Africa Development Community

SAGCOT	Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania
SDGs	Sustainable Development Goals
SEZ	Special Economic Zone
SIDO	Small Industry Development Organisation
SME	Small and Medium Enterprise
STI	Science, Technology and Innovation
TADB	Tanzania Agricultural Development Bank
TANCIS	Tanzania Customs Integrated System
TANESCO	Tanzania Electricity Supply Company
TAZARA	Tanzania – Zambia Railways Authority
TDV	Tanzania Development Vision
TRA	Tanzania Revenue Authority
TRL	Tanzania Railways Limited
TTCL	Tanzania Telecommunications Company Limited
UK	United Kingdom
USA	United State of America
USD	United States Dollar
VAT	Value Added Tax
WEO	Ward Executive Officers
WEO	World Economic Outlook



## **1.0 MABORESHO YA MIFUMO**

### **1.1 Utangulizi**

1. Serikali imeendelea kufanya maboresho ya Sheria, mifumo ya malipo na mifumo ya uandaaji wa mipango na bajeti katika jitihada za kuboresha usimamizi wa fedha za umma na kuboresha utoaji wa huduma. Baadhi ya maboresho ya hivi karibuni ni pamoja na:

#### **1.1.1 Maboresho ya Kisheria**

2. Bunge limefanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Umma Sura 348 kwa kuongeza kifungu cha 44 ili kuweka msukumo wa kisheria katika matumizi ya TEHAMA katika ukusanyaji wa fedha za umma. Aidha, sheria inamtaka kila Afisa Masuuli kusimamia matumizi ya Mfumo wa Malipo Mtandao Serikalini (*GePG*) katika ukusanyaji wa mapato.

#### **1.1.2 Matumizi ya TEHAMA katika Usimamizi wa Fedha za Umma**

3. Serikali imedhamiria kupunguza gharama za kiutawala na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, ulipaji wa mishahara pamoja na ununuzi wa bidhaa na huduma. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imeanzisha mifumo ifuatayo:-

##### **(i) Mfumo wa Malipo Mtandao Serikalini**

4. Mfumo huu mpya wa malipo ni mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia makusanyo yote ya mapato ya Serikali. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutumia mfumo huu ili kuongeza udhibiti katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali; kupunguza upotevu wa mapato; kuongeza ufanisi wa ukusanyaji; kuimarisha mfumo wa upatikanaaji wa taarifa sahihi za ukadiriaji wa mapato ya Serikali.

##### **(ii) Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (CBMS)**

5. Huu ni Mfumo mpya wa uandaaji na usimamizi wa bajeti kupitia wavuti unaboresha makisio ya bajeti, ugawaji wa rasilimali na taarifa za mwenendo na utekelezaji wa bajeti. Baadhi ya maboresho yamejumuisha uainishaji wa hesabu za kifedha, mapitio ya takwimu za kifedha za serikali (GFS) 2014, maoteo ya mtiririko wa fedha, utoaji wa hati za matumizi na uwekaji wa kumbukumbu za ahadi za miradi inayotekelezwa kwa zaidi ya mwaka mmoja. Mfumo unatarajiwa kupunguza muda unaotumika katika kuandaa bajeti na kutoa taarifa za utekelezaji. Mfumo huu utatumiwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Sekretariaeti za Mikoa katika uandaaji, utekelezaji na utoaji wa taarifa za kibajeti kuanzia mwaka 2018/19. Mfumo

huu utasitisha utumiaji wa mfumo wa *SBAS* uliokuwa ukatumika katika maandalizi ya bajeti

**(iii) Mfumo wa Kupanga Mipango Na Utoaji Taarifa kwenye Serikali za Mitaa**

6. Mfumo ulioboreshwa wa kupanga mipango na kutoa taarifa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ni mfumo ambao unatumika kwa njia ya wavuti na inaunganisha mifumo inayotumika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kama vile *IFMS – Epicor*, Mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali za mitaa, Mfumo wa Uhasibu na Ripoti, Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mfumo wa Taarifa za Afya katika Wilaya. Mfumo huu umezingatia kuongeza ufanisi, uwajibikaji na usahihi wa taarifa na uwazi katika kutekeleza Bajeti. Maboresho ya mfumo huu yamelenga kupima matokeo ya huduma ikilinganishwa na rasilimali zilizotumika.

**(iv) Mfumo wa Malipo ya Mishahara Serikalini**

7. Mfumo wa malipo ya mishahara Serikalini unatumia utaratibu wa kielektroniki wa kuhamisha fedha kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Serikali. Faida za Mfumo huu ni pamoja na; kurahisisha ulipaji wa mishahara, usalama, na kupunguza gharama kwa Serikali.

**(v) Mfumo wa Malipo baina ya Benki**

8. Huu ni mfumo wa kielektroniki wa malipo na usimamizi wa akaunti kwa njia ya ya mtandao na uhamisho wa miamala mikubwa ya fedha baina ya benki kwa wakati. Manufaa ya mfumo huu ni pamoja na:- kuondoa matumizi ya hundi, kurahisisha ufuatiliaji wa miamala na utoaji wa taarifa, kupunguza udanganyifu na kuwezesha uanzishwaji wa akaunti moja ya Hazina. Aidha, Mfumo huu umeboresha mfumo wa malipo kwa kupunguza muda uliokuwa ukatumika katika kukamilisha mialama mikubwa baina ya benki.

**1.2 Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano**

9. Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango unalenga kuimarisha ushirikiano baina ya wadau, kuongeza ufanisi na utendaji bora katika utekelezaji wa Mpango ili kufikia malengo ya taifa.

10. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia sheria, kutumia mifumo hii na Mkakati huu katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango na bajeti zao.

## **2.0 UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI**

### **2.1 Utangulizi**

11. Uandaaji wa Mpango na Bajeti una mchakato na ratiba yake ambayo inapaswa kuzingatiwa. Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na mashirika ya Umma zinapaswa kuwa na Mpango ambao unazingatia malengo na shabaha za Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango Mkakati wa taasisi. Mipango hii inapaswa kutafsiriwa katika bajeti ya utekelezaji kwa kila mwaka na maoteo ya muda wa kati. Maelekezo yanatolewa ili kuzingatiwa katika hatua mbalimbali za maandalizi ya mipango na bajeti za taasisi kwa mwaka 2018/19.

### **2.2 Ratiba ya uwasilishaji wa Mipango na Bajeti**

12. Maandalizi ya rasimu ya mpango na maoteo ya bajeti za Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma yanapaswa kuanza mapema mara baada ya Mwongozo huu kuidhinishwa kwa kuzingatiwa Muundo wa Bajeti ya Muda wa Kati (MTEFs). Kitabu cha Bajeti ya Muda wa Kati kiwasilishwe Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi wiki ya kwanza ya Mwezi Febuari, 2018. Vitabu vya Bajeti ya Muda wa Kati vya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, baada ya kupitishwa na mamlaka husika, vitawasilishwa kwenye OR-TAMISEMI wiki ya tatu ya Mwezi Januari, 2018 kwa ajili ya uchambuzi.

13. Wizara ya Fedha na Mipango itaratibu uchambuzi wa kitaalam na kufanya majumuisho ya bajeti za mafungu yote kwa ajili ya kuwasilisha kwenye Kamati za Kudumu za Bunge kwa Sekta husika. Aidha, Mafungu yataandaa randama za bajeti zao zitakazowasilishwa kwenye Kamati za Bunge kuanzia wiki ya tatu ya mwezi Machi, 2018 hadi wiki ya kwanza ya mwezi Aprili, 2018 kwa ajili ya uchambuzi wa vipaumbele vya kisera na ushauri. Majumuisho na ushauri wa Kamati za Bunge za Kisekta yatawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa kuanzia wiki ya pili ya mwezi Aprili hadi wiki ya nne ya mwezi Juni, 2018. Utekelezaji wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge utaanza tarehe 1 Julai, 2018 hadi tarehe 30 Juni, 2019.

### **2.3 Majadiliano na Kamati za Bajeti**

14. Maandalizi ya awali ya mipango na bajeti katika ngazi zote za Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma yanapaswa kuanza mara baada ya kuidhinishwa kwa mwongozo huu chini ya usimamizi wa Maafisa Masuuli. Rasimu ya mipango na

bajeti iwasilishwe kujadiliwa na kupitishwa katika Mabaraza ya Wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma SURA 105.

15. Kamati za Bajeti zina wajibu muhimu katika kufanikisha maandalizi ikiwemo uchambuzi wa awali wa bajeti za mafungu yao kama ilivyoanishwa katika Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015, kanuni ya 17(3). Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kuzingatia maelekezo hayo pamoja na nyaraka za Msajili wa Hazina. Aidha, Bajeti ya Muda wa Kati ziandaliwe na kuwasilishwa katika muundo ulioelekezwa kwenye kiambatisho.

#### **2.4 Mchakato wa Uchambuzi na Uwasilishaji wa Bajeti**

16. Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Msajili wa Hazina; na Wadau wengine watafanya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma kwa mujibu wa kifungu 22(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

17. Wakati wa Uchambuzi wa bajeti, Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinapaswa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango nakala ngumu mbili (2) na nakala laini ya rasimu ya mpango na bajeti kwa ajili ya uchambuzi wa kitaalamu na baada ya makubaliano watawasilisha nakala mbili ngumu zilizosainiwa na nakala laini kwa mamlaka husika. Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa pia kuwasilisha OR-TAMISEMI nakala ngumu moja (1) ya mpango na bajeti ya mwisho iliyosainiwa. Aidha, Taasisi za Umma na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kuwasilisha nakala ngumu nne (4) zilizosainiwa, kwa mgawanyo wa mbili (2) kwenda Wizara mama na mbili Ofisi ya Msajili wa Hazina.

#### **2.5 Uingizaji wa Takwimu kwenye Mfumo wa Bajeti**

18. Kwa kuzingatia ratiba ya maandalizi na uchambuzi wa Bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutekeleza yafuatayo:

- i. Kuhakikisha kwamba uingizaji wa takwimu kwenye mfumo wa bajeti unafanyika kwa usahihi na kwa wakati;
- ii. Kuzingatia Mfumo wa Serikali wa Takwimu za Kifedha toleo la mwaka 2014 kama ilivyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;
- iii. Kutumia vizio vilivyobainishwa kwenye mfumo wa CBMS; na



- iv. Kutumia vizio rasmi kufanya makadirio ya gharama za uendeshaji kama vile pango, umeme, maji na simu.

## **2.6 Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2018/19**

19. Maeneo ya kipaumbele na miradi itakayotekelezwa kwa mwaka 2018/19 ni kama yalivyobainishwa katika kitabu cha Mpango wa Pili wa Maendeleo na Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Aidha, kati ya vipaumbele vilivyoainishwa, maeneo yaliyopewa msukumo wa kipekee kwa mwaka 2018/19 ni pamoja na:

- i. **Umeme:** katika kufikia azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda, nishati ya umeme ni kichocheo na hitaji la msingi. Katika kufanikisha hilo, msukumo utawekwa kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini;
- ii. **Madini:** kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini, kuboresha usimamizi wa kodi ili kuziba mianya ya ukwepaji wa kodi katika sekta ya madini na kuwezesha shughuli za uchenjuaji nchini kwa ajili ya kuongeza thamani ya madini;
- iii. **Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji:** kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* kati ya Dar es Salaam na Morogoro na kuanza kwa kipande cha Morogoro hadi Makutopora ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika njia ya reli; uimarishaji wa viwanja vya ndege; na kuimarisha mtandao wa barabara;
- iv. **Kilimo:** kuimarisha kilimo kwa ajili ya upatikanaji wa uhakika wa chakula na malighafi za viwanda, kuendeleza maboresho ya miundombinu ya umwagiliaji, kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo, kuboresha utafiti wa kilimo na mbegu bora, kuboresha huduma za ugani, kuboresha usindikaji wa mazao na upatikanaji wa miundombinu ya hifadhi na masoko;
- v. **Mifugo na Uvuvi:** Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo ya uzalishaji bora wa mifugo ili kupata bidhaa za mifugo zenye ubora (ngozi na nyama); Uboreshaji wa masoko, miundombinu ya uzalishaji mifugo na kuongeza thamani bidhaa za mifugo; Kuimarisha na kuboresha shughuli za uvuvi katika bahari kuu na vyanzo vingine, ujenzi wa bandari za uvuvi, uhifadhi wa rasilimali bahari na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi;
- vi. **Afya:** Kujenga hospitali za mikoa katika mikoa mipya mitano, Kuimarisha taasisi za mafunzo ili kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali watu, kuzipatia vifaa na vitendanishi vya kutosha hospitali za rufaa, hospitali maalum na hospital ya Taifa; kuimarisha huduma kwa akinamama wajawazito na watoto; Kuimarisha huduma za upasuaji katika vituo vya afya; Kuboresha upatikanaji wa huduma za

madaktari bingwa; Kuboresha huduma na upatikanaji wa dawa kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI; kudhibiti mazalia na maambukizi ya malaria; na kuimarisha upatikanaji wa masoko kwa dawa zinazozalishwa nchini;

- vii. **Elimu:** kuendelea kuimarisha mazingira ya utoaji wa elimu katika ngazi zote; Kuimarisha udhibiti wa ubora wa elimu; Kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Elimumsingi bila malipo; Kuendela kujenga na kuimarisha vyuo vya ufundi stadi nchini; Kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; na Kuimarisha utafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu;
- viii. **Maji safi na Salama na Udhibiti wa Maji taka:** kusimamia vyanzo na ubora wa maji; Ujenzi wa Mabwawa ya kimkakati; Kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji nchini; Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa miundombinu ya maji safi na maji taka na huduma za maji safi na salama vijijini na mijini na maeneo ya biashara;
- ix. **Utalii:** ujenzi wa miundombinu wezeshi ya utalii; kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii nchini; kuanzisha maeneo ya kitalii na burudani (Theme Park); na kukuza utalii wa ufukweni;
- x. **Viwanda:** Kuanzisha na kuendeleza maeneo ya viwanda (Industrial parks) na maeneo ya Teknolojia (Technological Parks); Kupanua na Kuimarisha Shughuli za Shirika la Viwanda Vidogo – SIDO; Kuimarisha na kuzitumia taasisi za umma katika kuleta mageuzi ya viwanda nchini; na kuboresha upatikanaji wa mikopo.

20. Maafisa Masuuli wanaohusika na maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa hapo juu pamoja na mengine wanaelekezwa kuzingatia miradi hiyo katika maandalizi ya mipango na bajeti zao.

### **3.0 MFUMO WA MAPATO NA MATUMIZI**

#### **3.1 Utangulizi**

21. Sehemu hii inaelekeza namna ya kutayarisha makadirio ya mapato na matumizi na uzingatiaji wa ukomo wa bajeti kwa mwaka 2018/19. Mapato ya Serikali yanahusisha vyanzo vya kodi na visivyo vya kodi, misaada na mikopo ya ndani na nje. Upatikanaji wa rasilimali fedha ni muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Aidha, pana umuhimu wa kuimarisha makadirio ya matumizi kwa shughuli na kwa mafungu husika. Sehemu hii inaelekeza namna ya kutayarisha makadirio ya mapato na matumizi ya rasilimali fedha kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretariati za Mikoza na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia vigezo vilivyopo.

## **3.2 Mahitaji ya Rasilimali Fedha**

### **3.2.1 Mapato ya Ndani**

22. Kwa mwaka 2018/19, makadirio ya awali ya mapato ya ndani ni Shilingi bilioni 22,088.2, ambapo Shilingi bilioni 18,817.0 ni mapato ya kodi na Shilingi bilioni 2,423.5 ni mapato yasiyo ya kodi. Vile vile, mapato ya ndani ya Halmashauri ni Shilingi bilioni 847.7. Makadirio ya mapato yatatakiwa kuonesha mwenendo wa makusanyo, mapitio ya bajeti nusu mwaka, matarajio ya makusanyo na maoteo kwa mwaka wa kizio na miaka miwili inayofuatia katika kipindi cha muda wa kati kama inavyoelekezwa katika Kitabu cha Mwongozo (Manual) wa Uandaaji wa Mipango na Bajeti pamoja na Kiambatisho cha Mwongozo huu. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa pia kuzingatia yafuatayo:-

- i. Kuwasilisha makusanyo ya mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015;
- ii. Kufanya mapitio ya kodi, ada, tozo na ushuru pamoja na kubuni na kuanzisha vyanzo vipya vya mapato (kama urasimishaji wa biashara) ili kuongeza wigo wa mapato. Aidha, kuhakikisha kwamba makusanyo yanakusanywa kwa kupitia mifumo ya kielektroniki ili kudhibiti upotevu wa mapato; Vilevile Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutumia wakandarasi na watoa huduma wanaotumia mashine za kielektroniki za kukusanya mapato;
- iii. Kuepuka kuingia mikataba inayohusisha vipengele vya misamaha ya kodi bila idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango;
- iv. Kutumia vyanzo vya mapato vilivyobainishwa katika Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo kwa lengo la kuongeza mapato;
- v. Kuimarisha usimamizi wa vituo vya makusanyo hususan katika maeneo ya mipaka, viwanja vya ndege, Bandari pamoja na vituo vya ukaguzi;
- vi. Kupanga matumizi ya ardhi, kupima na kumilikisha ardhi;
- vii. Taasisi na Mashirika ya Umma yanayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 yanawasilisha mapato katika akaunti zilizopo Benki Kuu na kuendelea kutumia akaunti za uendeshaji katika benki za kibiashara;
- viii. Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyotakiwa kuwasilisha asilimia 15 ya mapato ghafi kuhakikisha mapato hayo yanawasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kuonesha makusanyo yote ya mapato kwenye MTEF zao; na
- ix. Kuingia mikataba ya kiutendaji na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB); Pia Taasisi na Mashirika ya Umma wataingia mikataba ya kiutendaji na Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma.

### **3.2.2 Misaada na Mikopo Nafuu**

23. Serikali inakadiria kupokea jumla ya Shilingi bilioni 3,658.2. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 946.0 ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, shilingi bilioni 2,153.3 ni misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 558.9 ni misaada na mikopo nafuu ya mifuko ya pamoja ya kisekta. Hata hivyo, mwenendo wa misaada na mikopo nafuu katika miaka ya hivi karibuni umekuwa chini ya ahadi. Kwa ajili ya kuimarisha makusanyo kutoka chanzo hiki, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

- i. Kukamilisha kwa wakati maandalizi ya maandiko ya miradi na majadiliano na Washirika wa Maendeleo;
- ii. Kukamilisha taratibu zote zinazotakiwa kwa idhini ya miradi kuingia katika bajeti ya Serikali kabla ya mwezi Februari 2018;
- iii. Kuhakikisha wanatimiza masharti waliokubaliana na Washirika wa Maendeleo;
- iv. Utoaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi kwa wakati; na
- v. Kuwa na mkakati wa usimamizi wa madeni na misaada katika robo ya kwanza ya mwaka.

### **3.2.3 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

24. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutekeleza miradi ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa mujibu wa Sheria ya Ubia Na. 18 ya Mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2014.

25. Bajeti ya utekelezaji wa miradi ya Ubia itazingatia uwepo wa taarifa za upembuzi yakinifu. Hivyo Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kukamilisha upembuzi yakinifu ili kuwezesha miradi hiyo kutekelezwa kupitia utaratibu wa ubia.

26. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma zinazotarajia kushirikiana na sekta binafsi katika miradi zinapaswa kufanya maandalizi ya kutosha ikiwemo upembuzi yakinifu kabla ya kuingia makubaliano ya kutekeleza miradi hiyo. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- i. Kubainisha miradi itakayovutia uwekezaji wa sekta binafsi na kuiwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi kwa mujibu wa Sheria ya Ubia Na. 18 ya Mwaka 2010 (pamoja na marekebisho yake). Kwa upande wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, miradi ya ubia inapaswa kuwasilishwa OR– TAMISEMI kwa ajili ya uchambuzi na uidhinishwaji kabla ya kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango;

- ii. Kujumuisha miradi ya Ubia katika mipango na mikakati ya sekta zao;
- iii. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango gharama za upembuzi yakinifu, pengo la kugharamia mradi (viability gap funding), gharama ya huduma zinazotolewa kwa mtoa huduma (availability payment) na dhamana inayohitajika ya miradi ya Ubia iliyo chini ya sekta zao ili ziweze kufanyiwa tathmini kwa ajili ya malipo;
- iv. Kuzingatia vigezo vya miradi ya Ubia ili kufikia sifa ya kupewa fedha vikiwemo: taarifa ya upembuzi yakinifu, uwezo wa kulipia wa gharama, thamani ya fedha, uhamishaji wa vihatarishi, kukidhi matakwa ya kiuchumi na kibiashara na mradi wenye kukidhi vigezo vya kifedha; na
- v. Katika kutekeleza, miradi ya kibiashara ipewe kipaumbele dhidi ya miradi ya kijamii.

### **3.3 Matumizi**

27. Maoteo ya matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/19 yanakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 32,476.0. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida ni Shilingi bilioni 20,227.6 ambayo yanajumuisha shilingi bilioni 7,627.7 za matumizi ya mishahara. Matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa jumla ya Shilingi bilioni 12,248.3. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 9,536.2 ni matumizi ya maendeleo kwa fedha za ndani.

#### **3.3.1 Matumizi ya Kawaida**

##### **a. Mishahara**

28. Maoteo ya bajeti ya mishahara yatazingatia:- watumishi waliopo, ajira mpya, upandishaji wa vyeo, nyongeza za mishahara na michango ya kisheria. Hivyo, katika uandaaji wa bajeti hiyo. Maafisa Masuuli watatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na OR-MUUUB pamoja na Ofisi ya Msajili wa Hazina katika kunda bajeti ya mishahara. Katika kuandaa Bajeti ya Mishahara yafuatayo lazima yazingatiwe:-

- i. Kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimali Watu kuandaa mipango na bajeti ya mwaka 2018/19;
- ii. Malipo ya mishahara yazingatie maelekezo ya Waraka wa Hazina Na.2 wa Mwaka 2017 unaoelekeza utumiaji wa *Government Salary Payments Platforms* (GSPP);
- iii. Posho za kukaimu nafasi za uongozi zinazosubiri uteuzi zilipwe kupitia bajeti za mishahara. Aidha, posho za kukaimu nafasi za uongozi zinazotokana na ugonjwa, likizo na safari zitaendelea kukasimiwa katika bajeti ya matumizi mengineyo. *Waraka wa Utumishi* Na. 1 wa Mwaka 2015 unatoa maelekezo zaidi;
- iv. Kuendelea kufanya uhakiki wa takwimu za watumishi na kuondoa wasiostahili, pamoja na kufanya tathmini ya mahitaji ya watumishi kwa mujibu wa ikama; na

- v. Kutenga bajeti kwa ajili ya michango ya Kisheria pamoja na kiinua mgongo kwa watumishi wenye ajira za mikataba.

29. Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na OR-MUUUB na OTR wakati wa kuandaa bajeti ya mishahara.

**b. Matumizi Mengineyo**

30. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga fedha kwa ajili ya matumizi yasiyoepukika pamoja na majukumu ya msingi wakati wa utayarishaji wa bajeti ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali ya watumishi pamoja na madeni ya wazabuni na watoa huduma mbalimbali ili kuepuka kulimbikiza madeni na gharama za kulipa riba.

**c. Ruzuku kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**

31. Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaendelea kupokea ruzuku kutoka Serikali kuu ili kuziwezesha kutekeleza majukumu ya utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa ufanisi zaidi. Ruzuku hizo zinatolewa kwa mfumo wa Ruzuku ya Maendeleo isiyoyamasharti, Ruzuku za maendeleo za kissekta pamoja na fedha za Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida. Utoaji wa ukomo wa bajeti kwa Serikali za Mitaa utazingatia vigezo vya kissekta vya ugawaji rasilimali fedha. Aidha, vigezo hivyo vitajumuisha gharama za utoaji wa elimu msingi bila malipo; ruzuku ya uendeshaji wa shule (Capitation) kwa Shule za awali, Msingi na Sekondari; chakula cha wanafunzi; shule zenye mahitaji maalum; na posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari na Waratibu Elimu Kata. Sura ya 2 ya Mwongozo huu inatoa maelekezo zaidi kuhusu ugawaji wa rasilimali fedha kwa Wizara, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**3.3.2 Bajeti ya Maendeleo**

32. Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinapaswa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21 katika mchakato wa kuandaa mipango ya maendeleo na makadario ya bajeti. Maafisa Masuuli pia wanaelekezwa kutumia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Miradi ya Umma wakati wa kuandaa miradi ya uwekezaji. Hivyo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

- i. Kuendelea kutekeleza Sera ya Ugatuuji wa Madaraka kwa kuhakikisha kuwa fedha zinatengwa kwenye Halmashauri husika badala ya kutengwa kwenye bajeti za Wizara;
- ii. Kutenga fedha za utekelezaji wa miradi ambayo imepitishwa na kuidhinishwa na Wizara ya Fedha na Mipango;

- iii. Maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa kwenye mwongozo huu na maeneo mengine ya kimkakati yaliyoainishwa katika Mpango kazi wa Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
- iv. Mkakati wa Mawasiliano, Ugharimiaji, na Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
- v. Kutenga fedha kwa miradi ya maendeleo ambayo utekelezaji wake unaendelea;
- vi. Kufanya uthamini wa ardhi na mali pamoja na kulipa fidia katika maeneo ya kimkakati kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda;
- vii. Kutoa kipaumbele katika kufanya tafiti za viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini;
- viii. Kuwezesha uanzishaji wa kongane za viwanda na upatikanaji wa teknolojia rahisi na nafuu;
- ix. Kulipa madeni ya makandarasi kwa wakati ili kuepuka ongezeko la deni kutokana na riba na tozo;
- x. Kuhakikisha uwepo wa miundombinu wezeshi kwa uwekezaji wa viwanda;
- xi. Kuandaa miradi ya kimkakati kwa kuzingatia matakwa ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/19;
- xii. Kuweka bayana matumizi ambayo yatahitaji kulipiwa kwa fedha za kigeni na kiwango cha fedha ambacho kitahitajika (Fomu Na.11B (D)); na
- xiii. Kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini.

33. Wizara ya Fedha na Mipango itahakiki na kuidhinisha miradi inayotekelezwa kwa zaidi ya mwaka mmoja kulingana na Kifungu Na. 51 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 na Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi Na. 18 ya Mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2014. Vilevile, ugawaji wa ruzuku ya maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa utazingatia vigezo vilivyoainishwa kwenye Mwongozo Ulioboreshwa wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

34. Bajeti ya maendeleo ya miradi na programu zinazotumia fedha za nje itaandaliwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma baada ya kupata uthibitisho wa ahadi zilizotolewa na Washirika wa Maendeleo. Hivyo, ni muhimu kwa Maafsa Masuuli kuzingatia yafuatayo:-

- i. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango mikataba ya miradi inayopokea ufadhili wa fedha za nje;
- ii. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya siku 30 baada ya robo mwaka husika kuisha;

- iii. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa ya utekelezaji ya mwaka kabla ya tarehe 15 Oktoba baada ya mwaka wa fedha husika kumalizika;
- iv. Kujumuisha kwenye bajeti mchango wa Serikali kwa miradi ya maendeleo inayogharamiwa kwa fedha za Nje;
- v. Miradi inayotumia fedha za Washirika wa Maendeleo ioneshwe kwenye makadirio ya bajeti; na
- vi. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa ya kila robo mwaka ya fedha, vifaa na utaalum kwa miradi inayopata ufadhili wa moja kwa moja kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

### **3.4 Vigezo vya Ugawaji wa Rasilimali Fedha**

35. Vigezo vya kugawa rasilimali fedha vitazingatia aina ya matumizi ya shughuli za Serikali (Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo) pamoja na majukumu ya msingi ya Taasisi husika.

36. Wizara ya Fedha na Mipango itatoa viwango vya ukomo wa bajeti kwa Mafungu yote ya Wizara, Idara Zinzotegemea na Wakala wa Serikali, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia vigezo kama vilivyobainishwa katika Mwongozo huu. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia viwango vya ukomo wa bajeti vilivyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/19. Aidha, wanaelekezwa kupanga bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vya Mafungu husika. Vile vile, inasisitizwa kwamba hakutakuwa na nyongeza ya ukomo wa bajeti nje ya viwango vilivyotolewa.

## **4.0 MAMBO MENGINE YA KUZINGATIWA KATIKA UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI**

### **4.1 Kudhibiti Ulimbikizaji wa Madeni**

37. Ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Kifungu cha 52 (1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 na Waraka wa Mlipaji Mkuu wa Serikali Na. 4 wa 2014. Hivyo, wanaagizwa:

- i. Kuhakikisha madeni yote yamehakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali;
- ii. Kuweka kipaumbele katika utengaji wa fedha za kulipia madeni yaliyohakikiwa;
- iii. Kuhakikisha hakuna miradi mipya inayoanzishwa bila kuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi hiyo; na
- iv. Kufanya miadi yote kupitia Mfumo wa Malipo wa Serikali.



## **4.2 Madeni Sanjari**

38. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kufuatilia kwa ukaribu mikataba inayoweza kusababisha madeni sanjari na kutenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni yaliyopo. Pia madeni sanjari yaliyopo yaonekane kwenye hesabu za mwisho wa mwaka.

## **4.3 Kudhibiti Matumizi na Kupunguza Gharama**

39. Maafisa Masuuli wanapaswa kusimamia nidhamu ya matumizi ya Fedha za Umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma SURA 348, Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa SURA 290, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 SURA 410 na kanuni husika, pamoja na miongozo mbalimbali ya Serikali bila kuathiri huduma zinazotolewa. Hivyo, wanaelekezwa:

- i. Kuhakikisha Mikataba yote inakuwa katika Shilingi za Kitanzania ili kupunguza athari za madiliko ya viwango vya ubadilishaji fedha, isipokuwa kwa mikataba inayohusisha makampuni ya kimataifa;
- ii. Kuendelea kupunguza gharama na matumizi yasiyokuwa ya lazima kwa kutumia kumbi za Serikali kwa mikutano yote ikiwa ni pamoja na mikutano ya bodi, mafunzo, warsha na semina;
- iii. Kuhakikisha Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyoanzishwa kwa lengo la kujiendesha kibiashara, yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali;
- iv. Kuhakikisha thamani halisi ya fedha inazingatiwa katika manunuzi ya bidhaa, huduma na ujenzi;
- v. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mifumo ya matumizi ya umma (maji, simu na umeme) ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia inayopunguza matumizi ya nishati ili kudhibiti gharama;
- vi. Kufanya uhakiki wa wafanyakazi mara kwa mara ili kuhakikisha mishahara inalipwa kwa watumishi wanaostahili;
- vii. Kuhakikisha balozi na makazi ya wawakilishi walioko nje ya nchi wanatumia utaratibu wa kulipia kwa awamu (mortgage financing arrangement) katika kununua majengo badala ya utaratibu wa kupanga;
- viii. Kuendelea na utaratibu wa kutumia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini kwenye ununuzi wa magari;
- ix. Kuhakikisha mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu inatolewa kwa waliokidhi vigezo; na
- x. Kutumia mfumo wa Serikali Mtandao kwa mawasiliano baina ya Ofisi za Serikali.

#### **4.4 Kiwango cha Ubadilishaji Fedha**

40. Katika kuandaa Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19, kiwango cha ubadilishaji fedha kitakachotumika kubadilisha fedha za kigeni kwa Shilingi za Tanzania itakuwa Dola moja ya Marekani kwa Shilingi za Tanzania 2,308.5.

#### **4.5 Kujumuisha Masuala Mtambuka Katika Mipango na Bajeti**

41. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga fedha katika mwaka 2018/19, kwa ajili ya kutekeleza masuala mtambuka kama vile: Jinsia, UKIMWI na Virusi vya UKIMWI, Watu wenye Ulemavu, Idadi ya Watu, Kinga ya Jamii, Ulinzi wa Mtoto, Vijana na Wazee, na mazingira. Aidha, shughuli hizo zizingatie miongozo ya kujumuisha masuala mtambuka katika mipango na bajeti;

42. Maafisa Masuuli wanaohusika na utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18-2021/22) wahakikishe kuwa bajeti zao za mwaka 2018/19 zinajumuisha kazi zilizoainishwa katika mkakati huo.

43. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga fedha za kwa ajili ya maboresho ya utawala bora, utoaji huduma na uwajibikaji. Maboresho haya yanajumuisha Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Tano, Maboresho katika Serikali za Mitaa, Maboresho ya Sekta ya Fedha, Udhhibiti wa Fedha Haramu, Mfumo wa Nchi za Kiafrika wa Kujitathmini zenyewe na Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu. Maboresho mengine ni pamoja na kutokomeza Rushwa, Kuhamasisha Uongozi Imara, Kuboresha Mazingira ya Biashara, Utawala wa Ardhi, na Maboresho yanayoweza Urasimishaji wa mali, Kuwezesha Serikali kuwa na Ufanisi zaidi na Kuimarisha Ushiriki wa Wananchi kupitia Maendeleo ya Kiuchumi katika ngazi ya Jamii. Kwa msingi huo, kila taasisi inapaswa kuandaa programu na kutenga rasilimali kwa ajili ya kutekeleza Maboresho husika.

44. Maafisa Masuuli ambao ni wajumbe wa Kamati ya Uendeshaji wa masuala ya Lishe (HLSCN) wanatakiwa kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza mikakati ya lishe kama ilivyoainishwa kwenye Mkakati Jumuishi wa Kitaifa kuhusu Lishe (2016/17-2020/21).

45. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kuzingatia vipaumbele vinavyohusu mazingira na mabadiliko ya tabia nchi katika bajeti zao kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Mkakati wa Kitaifa kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi kama ifuatavyo:

- i. Kufanya tathmini ya kimkakati ya athari za mazingira kwa lengo la kutenga fedha za kukabiliana na athari za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi;
- ii. Kuhakikisha kuwa tathmini ya athari za mazingira zinafanyika wakati wa kuandaa sera na program ambazo zinaweza kuwa na athari kubwa za mazingira. Gharama za kufanya tathmini hizo ziwekwe kwenye bajeti zao;
- iii. Miradi mikubwa yote itatakiwa ifanyiwe tathmini ya mazingira kama sehemu ya mipango na kuhakikisha kuwa bajeti zinatengwa kwa ajili ya kupunguza athari hasi za mazingira;
- iv. Kuhakikisha wanafuatilia viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Bajeti ziakisi mazingira endelevu.

#### **4.6 Ushirikiano wa Kimataifa na Kikanda**

46. Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaagizwa kuzingatia yafuatayo:
  - i. Kufuata Maelekezo ya Mfumo wa Ushirikiano wa Kimaendeleo (DCF) katika kutekeleza makubaliano na mikataba mbalimbali kati ya Tanzania na nchi nyingine;
  - ii. Kuhakikisha masuala ya EAC, SADC na makubaliano mengine ya kikanda yanajumuishwa katika mipango na bajeti zao;
  - iii. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango michango ya kuchangia Taasisi za Kimataifa na Kikanda kwa ajili ya kujumuishwa, kutengewa fedha na kulipwa kwa pamoja;
  - iv. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango mchango wa Serikali katika miradi ya maendeleo inayofadhiiwa na washirika wa maendeleo (counterpart fund) kwa ajili ya kutengewa fedha;
  - v. Kuhamasisha umma kwa kushirikiana na wadau wengine kuhusu fursa zilizopo katika mipango ya ushirikano wa Kikanda na Kimataifa; na
  - vi. Kuendelea kujenga uwezo wa maofisa hususan waliopo katika balozi za Tanzania ili kushiriki ipasavyo kwenye mikutano ya kikanda na kimataifa, hususani masuala ya kiuchumi.

#### **4.7 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma**

47. Mashirika na Taasisi za Umma lazima yajiendeshe kwa ufanisi ili kuboresha utoaji wa huduma na kupata faida na kuchangia sehemu ya mapato kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kulingana na matakwa yaliyopo. Aidha, Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma uende sambamba na kuhakikisha dhana ya Utawala bora inatekelezwa pamoja

na kuzingatia mifumo ya uendeshaji wa Taasisi ikiwemo Sheria, Kanuni na Taratibu kwa lengo la kuboresha huduma iliyokusudiwa.

48. Katika kuzingatia hayo, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaelekezwa kuhakikisha kuwa:

- i. Maafisa Masuuli wa Taasisi na Mashirika ya Umma wanapunguza matumizi yasiyo na tija kwa lengo la kuwa na utendaji wenye Ufanisi kwenye Mashirika na Taasisi za Umma. Hivyo, wahakikishe kuwa mapato yasiyo ya kodi yatokanayo na mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi kwa mashirika yenye vigezo yanawasilishwa kwa wakati katika kila robo mwaka;
- ii. Mashirika ya Umma yanalipa gawio la Serikali linalotokana na uwekezaji. Kwa Mashirika mengine ambayo Serikali ina hisa chache, Ofisi ya Msajili wa Hazina inayafuatilia ipasavyo;
- iii. Ushirikiano na Maafisa Masuuli wa Wizara mbalimbali za Kisekta unaendelezwa ili kuhakikisha dhana ya utawala bora na mifumo ya uendeshaji wa Taasisi inazingatiwa hususani uteuzi wa Wajumbe wa Bodi wenye sifa zinazohitajika kulingana na majukumu ya Taasisi husika;
- iv. Uchunguzi yakinifu umefanyika ili kuishauri Serikali kuhusu mifumo na majukumu ya Mashirika na Taasisi za Umma na kuishauri Serikali namna bora ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina SURA 370, Kifungu 10 (2b);
- v. Kushirikiana na Wizara za Kisekta kufuatilia Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa ili kubaini kama bado yanafanya kazi. Utaratibu wa kuwapata wawekezaji wengine watakaokuwa na uwezo wa kuyafufua na kuyaendeleza ikiwemo Mifuko ya Hifadhi za Jamii upewe msukumo wa kipekee. Aidha, hatua za ziada ikiwemo kurejesha Serikalini zichukuliwe kwa Wamiliki wa Mashamba na Viwanda watakaobainika kukiuka mikataba ya mauzo; na
- vi. Uhakiki wa mali zinazomilikiwa kwenye Mashirika na Taasisi za Umma unafanyika kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, kwa lengo la kuzibaini na kuweka taarifa na kumbukumbu sahihi.

#### **4.8 Usimamizi wa Vihatarishi**

49. Waraka wa Hazina Na. 12 wa mwaka 2012/13 unawataka Maafisa Masuuli kuandaa na kutekeleza mfumo wa usimamizi wa vihatarishi katika mafungu yao. Hivyo, wanaelekezwa kuhakikisha kuwa hatua za kukabiliana na vihatarishi zinajumuishwa katika mipango na bajeti zao kwa kuandaa malengo mahsusi kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo wa usimamizi wa vihatarishi.

## **5.0 MAELEKEZO MAHSUSI KWA SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA**

50. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Sekreariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wataendelea kutekeleza jukumu lao la msingi la kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa Wananchi. Kwa msingi huo, wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:-

- i. Maandalizi ya Mipango na Bajeti na utekelezaji utafanyika kupitia mfumo wa PlanRep isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo;
- ii. Mipango na Bajeti izingatie takwimu sahihi na za uhakika;
- iii. Kudumisha amani, utulivu na usalama katika maeneo yao ya Utawala;
- iv. Kuandaa Bajeti ya maandalizi pamoja na ya uchaguzi wa viongozi katika ngazi za msingi kwa mwaka 2019 kwa kuainisha kwa ufasaha kazi zitakazofanyika na kuingiza kwenye Mpango na Bajeti;
- v. Kuhakikisha Mikutano ya kisheria inafanyika na kuweka maazimio katika maeneo ya wazi na katika tovuti za kila Halmashauri na Mikoa hususan taarifa za mapato na matumizi za ngazi za Kata na Kijiji/Mtaa;
- vi. Kujiimarisha katika ujenzi, ukarabati na kuweka vifaa na vitendea kazi katika maeneo ya Utawala yaliyokwisha anzishwa;
- vii. Kuainisha makazi na shughuli mbalimbali zinazofanyika katika vyanzo vya maji, misitu ya hifadhi na maeneo mengine ya hifadhi na kuandaa Mikakati wa kuondoa makazi hayo kwa utaratibu mzuri;
- viii. Kuendelea kufanya mapitio ya Mipango Mikakati kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 ya Chama Tawala, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano pamoja na Mpango Mkakati wa OR – TAMISEMI na kuuweka katika tovuti;
- ix. Kufanya Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Ugatuuji Madaraka kwa Wananchi kwa kuhakikisha shughuli na fedha zilizogatuliwa kwenda kwenye ngazi za Kata, Kijiji/Mtaa zinasimamiwa ili kuboresha huduma za jamii na kuleta matokeo yanayolingana na malengo ya thamani ya fedha.
- x. Kutilia Mkazo Matumizi ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 kwa kuimarisha Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika maeneo ya Mijini na Vijijini pamoja na kushughulikia migogoro ya Ardhi pamoja na kutenga ardhi kwa ajili ya Viwanda na shughuli za ujasiliamali mdogo, wa kati na mkubwa na kuhakikisha maeneo hayo yanawekewa miundombinu muhimu;
- xi. Kuimarisha matumizi ya Mifumo ya Kielekroniki ili kuboresha utoaji wa huduma hususani matumizi ya vifaa vya kielekroniki katika ukusanyaji wa mapato na

- kudhibiti matumizi, matumizi ya tovuti za Serikali na mifumo ya upangaji mipango na utoaji taarifa ili kuongeza ufanisi, uwazi, uwajibikaji na kuhabarisha Umma juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Serikali;
- xii. Kuelimisha wafugaji juu ya njia bora za ufugaji ili kuwa na idadi ya mifugo michache yenye ubora na wanayoiumudu, kuzalisha ngozi bora kwa ajili ya usindikaji pamoja na kuzuia migogoro kati ya wakulima na wafugaji;
  - xiii. Kuhakikisha asilimia arobaini (40%) mpaka sitini (60%) ya mapato ya ndani ya Halmashauri yanapangwa na kutumika katika Miradi ya Maendeleo. Kipaumbele kitolewe katika kuwekeza ili kuimarisha vyanzo vikuu vya mapato katika Halmashuri (kilimo, uvuvi, biashara nk) ili kuimarisha vyanzo hivyo na kuwa na mapato endelevu;
  - xiv. Kutenga asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya; mfuko wa maendeleo wa Vijana (4%), Wanawake (4%) na watu wenye ulemavu (2%) na kusimamia utekelezaji;
  - xv. Kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya kijamii na kiuchumi katika sekta zote, hususani kujenga, kuboresha na kuweka vituo vya afya, vifaa madarasa, nyumba za watumishi, vyoo, maabara za sayansi, hosteli na mabweni. Kipaumbele kitolewe kwenye miradi ambayo haijakamilika hususan iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi;
  - xvi. Kuendeleza ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa Ofisi na Makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Ofisi za Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji na Mitaa;
  - xvii. Fedha zilizovuka mwaka zitumike kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya 2015 sehemu ya 29 (3) na kanuni za 2015;
  - xviii. Kuimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na kuanzisha mazao mbadala ili kupunguza hasara pamoja na kuwezesha viwanda vya usindikaji;
  - xix. Kuonesha madeni ya mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na kuiweka katika Mipango ya muda wa kati kupitia mfumo wa PlanRep ili kuwezesha marejesho kufanyika kulingana na mtiririko wa marejesho uliopitishwa na kutoa michango ya akiba;
  - xx. Kwa kuwa mchakato wa kuandaa mipango na bajeti unaanzia kwenye ngazi za vituo vya kutolea huduma (shule, zahanati na vituo vya Afya), mipango izingatie kuainisha namba ya kituo ili kuwezesha uchambuzi wa bajeti kulingana na akaunti ambayo imepokea fedha (ngazi ya kituo au Halmashauri);
  - xxi. Kuboresha mazingira ya kazi kwa Watumishi Umma kwa kutoa vitendea kazi na mafunzo;

- xxii. Kuhakikisha masuala ya utunzaji wa mazingira yanazingatiwa kwa ufasaha wakati wa kuandaa Mipango na Bajeti na katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- xxiii. Kuzingatia masuala ya ulinzi na usalama wa mtoto, lishe na ustawi wa Jamii katika mipango na bajeti;
- xxiv. Kujumuisha mahitaji ya makundi ya watu walio katika mazingira magumu na wenye mahitaji maalumu katika mipango na bajeti kulingana na Sera, Sheria na Miongozo iliyopo; na
- xxv. Kuiwezesha TARURA kutekeleza majukumu yake ya msingi.

### **5.1 Maelekezo Maalum kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Kuandaa na Kuwasilisha Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato**

51. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinahimizwa kubuni na kutekeleza miradi ya kimkakati ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kupunguza utegemezi kwa Serikali Kuu. Katika kufikia azma hiyo Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa:-

- i. Kuainisha na kupanga bajeti kwa miradi ya kimkakati itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/19 yenye lengo la kuongeza mapato. Mfano wa miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa standi za mabasi, masoko, maeneo ya maegesho, machinjio, miundombinu mbalimbali ya kutolea huduma pamoja na fursa zilizopo katika sekta mbalimbali;
- ii. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango miradi hiyo kwa ajili ya uchambuzi ili iweze kufikiriwa kupatiwa fedha kwa mwaka 2018/19. Vigezo vifuatavyo vinapaswa kuzingatiwa: -
  - a) Miradi hiyo iwe imejumuishwa katika mipango mikakati ya Halmashauri na katika MTEF;
  - b) Miradi yenye maandiko na taarifa za upembuzi yakinifu;
  - c) Miradi yenye uhakika wa fursa za kuongeza mapato;
  - d) Miradi ambayo Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa na uwezo wa kuiendesha zenyewe au kwa ubia;
  - e) Miradi ambayo inaongeza mnyororo wa thamani, vifungashio na mwingiliano endelevu wa viwanda (sustainable industrial integration); na
  - f) Miradi inayoongeza fursa za ajira, mapato na ustawi wa wananchi.

## **6.0 UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI**

### **6.1 Utangulizi**

52. Mafanikio ya Mpango na Bajeti kwa kiasi kikubwa yanategemea muundo wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa. Jambo hili linapewa msisitizo wa kipekee katika mwaka wa fedha 2018/19.

### **6.2 Ufuatiliaji na Tathmini**

53. Ufanisi wa ufuatiliaji na tathmini unategemea Mpango na Bajeti ulioandaliwa kwa kuzingatia viashiria, vigezo na shabaha bayana. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo, mipango na mikakati inabuniwa na kuwekewa viashiria, vigezo na shabaha bayana ambavyo usimamizi wa utekelezaji utavizingatia. Kwa mujibu wa Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, miradi mingi imepewa vigezo, viashiria na shabaha ili kufikia matokeo dhahiri na raslimali fedha za umma zinapangwa kwa umakini na usahihi kwa mujibu wa bajeti zilizoidhinishwa. Maandalizi ya Mpango na Bajeti yanapaswa kuzingatia vigezo hivyo.

54. Baada ya bajeti kuidhinishwa, Wizara, Idara Zinazojitgemea na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mkoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika na Taasisi za Umma zinaelekezwa:

- i. Kuandaa Mpangokazi wa utekelezaji wa bajeti na mtiririko wa fedha;
- ii. Kuzingatia Mfumo wa Muda wa Kati wa Matumizi;
- iii. Kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2015;
- iv. Kuzingatia Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II-MES) wakati wa kuanda mipango na bajeti na kufuatilia utekelezaji wake;
- v. Kutenga fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za ufuatiliaji na tathmini; na
- vi. Kutenga fedha kwa ajili ya kujenga uwezo na ujuzi wa ufuatiliaji na tathmini kwa rasilimali watu.

### **6.3 Taarifa za Utekelezaji**

55. Kwa mujibu wa Kifungu cha 55 (4) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni ya 30(5), Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini kwa utekelezaji uliofanyika ndani ya siku 30 baada ya kumalizika kwa kila robo mwaka. Pia, wanatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za mwaka za utekelezaji ifikapo tarehe 15 Oktoba baada ya kumalizika mwaka wa fedha.



56. Maafisa Masuuli pia wanaelekezwa:
- i. Kuwasilisha taarifa za utekelezaji za robo mwaka na za mwaka katika nakala ngumu na laini kwa Wizara ya Fedha na Mipango, OR-MUUUB, OR-TAMISEMI (kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamkala za Serikali za Mitaa) na Ofisi ya Msajili wa Hazina (kwa Mashirika na Taasisi za Umma); na
  - ii. Kuandaa, kutekeleza na kutoa taarifa za utekelezaji kwa kuzingatia muundo wa taarifa kama ulivyoainishwa katika Kiambatisho.

## **7.0 HITIMISHO**

57. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Mwongozo huu na Kiambatisho, na kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 na Kanuni za Bajeti za mwaka 2015 pamoja na nyaraka na miongozo mingine ya Serikali.



## **SEHEMU II**

### **MAPITIO NA MWELEKEO WA BAJETI**



## **SURA YA KWANZA**

### **MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA UCHUMI**

#### **1.1 Usuli**

1. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2012-2016), uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara ambapo ulikua kwa wastani wa asilimia 6.7 ukichagizwa zaidi na kuimarishwa kwa miundombinu ya usafirishaji, mawasiliano, ujenzi na huduma za fedha. Katika mwaka 2016, uchumi ulikua kwa asilimia 7.0, ikiwa ni asilimia 0.2 pungufu ya lengo lililowekwa la asilimia 7.2 kutokana na kuzorota kwa ukuaji wa sekta ya kilimo ambayo ina mchango mkubwa wa asilimia 28.9 katika Pato la Taifa. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 7.0 mwaka 2017 na kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 7.4 katika kipindi cha muda wa kati. Makadirio haya ya ukuaji yanatokana na matarajio ya kutekeleza kikamilifu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

2. Mfumuko wa bei umeendelea kubakia katika wigo wa tarakimu moja, hali iliyochangiwa na kuongezeka kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na ya nchi jirani, kuimarika kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan bei za mafuta ya petroli, na utekelezaji wa sera za bajeti za kupunguza matumizi. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani imeendelea kuwa imara kwa kipindi chote cha mwaka 2016/17 kuendana na hali ya ukwasi katika uchumi na kuimarika kwa urari wa malipo ya kawaida. Nakisi katika urari wa malipo ya kawaida ilipungua kwa kiasi kikubwa kufikia Dola milioni 1,353.3 mwaka 2016/17 kutoka Dola milioni 2,954.2 mwaka 2015/16, kutokana na kupungua kwa kiasi kikubwa kwa bidhaa na huduma ziliazoagizwa kutoka nje.

3. Katika mwaka 2016/17, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 6.1 mwezi Juni 2017 ikilinganishwa na asilimia 12.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulipungua kutoka asilimia 19.1 Juni 2016 hadi asilimia 1.3 mwezi Juni 2017. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na tahadhari iliyochukuliwa na benki za biashara katika kutoa mikopo kwa sekta binafsi kufuatia kuongezeka kwa mikopo chechefu. Pamoja na changamoto hiyo, sekta ya benki nchini iliendelea kuwa imara ikiwa na mitaji na ukwasi ulio juu ya viwango vinavyokubalika kisheria. Kupungua kwa mikopo kwa sekta binafsi kunaweza kupunguza fedha za uwekezaji kwa sekta binafsi na biashara na hatimaye kuathiri ukuaji wa uchumi. Katika kukabiliana na changamoto ya ukwasi katika uchumi, Serikali kupitia

Benki Kuu ya Tanzania ilipunguza kiwango cha amana ambacho benki za biashara zinatakiwa kuhifadhi Benki kuu kama dhamana (Statutory Minimum Reserve Requirement – SMR) na riba ambazo benki za biashara hulipa zinapokopa Benki Kuu (Discount Rate) kwa lengo la kuongeza ukwasi katika benki za biashara na hivyo kuziwezesha kukopesha sekta binafsi kwa gharama nafuu zaidi kwa ajili ya kuhamasisha shughuli za kiuchumi. Vile vile, Serikali imeendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu kwa lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji wa sekta binafsi.

## **1.2 Mwenendo wa Viashiria vya Uchumi**

### **1.2.1 Viashiria vya Ndani vya Uchumi**


#### **Ukuaji wa Pato la Taifa**

4. Pato halisi la Taifa liliendelea kuwa imara katika kipindi cha kuanzia mwaka 2012 hadi 2016 ambapo uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.7. Mwaka 2016, uchumi ulikua kwa asilimia 7.0 ukichangiwa na kuongezeka kwa ufuaji wa umeme hususan kwa kutumia gesi asilia, kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani, kuimarika kwa sekta ya usafirishaji, na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali katika sekta ya elimu kutokana na kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza na wa kidato cha kwanza kufuatia utekelezaji wa sera ya elimu-msingi bila malipo iliyoanza rasmi Januari 2016.

5. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.8 ikilinganishwa na asilimia 7.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni pamoja na: uchimbaji madini na mawe (asilimia 26.1); habari na mawasiliano (asilimia 13.0); usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 11.3); na ujenzi (asilimia 8.6). Sekta za usafirishaji na elimu pia zilikuwa na kasi ndogo ya ukuaji kufuatia kukamilika kwa shughuli ambazo zilikuwa ni za mara moja (*one off activities*) kwa mwaka 2016 ambazo ni kuanza kwa usafirishaji wa abiria kwa kutumia mabasi yaendayo haraka, usafirishaji wa gesi kupitia bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam na utekelezaji wa Sera ya elimu-msingi bila malipo.

6. Hata hivyo, kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 kulichangiwa zaidi na shughuli za fedha na bima kutokana na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi; kupungua kwa uzalishaji wa umeme kulikotokana na kumalizika kwa muda wa baadhi ya mikataba ya uzalishaji wa umeme; na kupungua kwa uzalishaji wa shaba katika robo ya pili ya mwaka 2017.

### Kielelezo Na. 1.1: Ukuaji wa uchumi kwa baadhi ya sekta (%)



### 1.2.2 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

7. Pato la Taifa la Tanzania limeendelea kukua kwa kiwango kikubwa kuliko nchi nyingine za Jumuiya. Ukuaji wa Pato la Taifa la Kenya ulifikia asilimia 5.8 mwaka 2016 ukiwa umeongezeka kutoka asilimia 5.7 mwaka 2015 ukichangiwa zaidi na sekta za ujenzi, uzalishaji viwandani, huduma za fedha na TEHAMA. Kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa la Rwanda ilipungua kufikia asilimia 5.9 mwaka 2016 kutoka asilimia 8.9 mwaka 2015 kutokana na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa katika soko la Dunia sambamba na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kupunguza ukwasi. Ukuaji wa Pato la Taifa la Uganda ulipungua kufikia asilimia 2.3 mwaka 2016 kutoka asilimia 5.7 mwaka uliotangulia. Burundi imeendelea kuwa na kasi ndogo ya ukuaji miongoni mwa nchi za Jumuiya ikiwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.0 mwaka 2016 kutoka ukuaji hasi wa asilimia 4.1 mwaka 2015. Jedwali Na. 1.1 linaonesha mwenendo wa ukuaji wa Pato la Taifa kwa nchi za Afrika Mashariki.

### Jedwali Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

	2014	2015	2016
Tanzania	7.0	7.0	7.0
Kenya	5.4	5.7	5.8
Uganda	4.6	5.7	2.3
Rwanda	7.6	8.9	5.9
Burundi	4.5	-4.0	-1.0


Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa, Oktoba 2017

## Mwenendo wa Mfumuko wa Bei

### (i) Mfumuko wa Bei Tanzania

8. Mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika kiwango cha tarakimu moja kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2017 ukichagizwa na sera madhubuti za kibajeti, kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan bei ya mafuta, na kasi ndogo ya ongezeko la bei za bidhaa za chakula katika soko la ndani. Hata hivyo, kwa kulinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2016, mfumuko wa bei uliongezeka kwa kiwango kidogo. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 5.8 ikilinganishwa na asilimia 5.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2016, wakati mfumuko wa bei za chakula ulikuwa wastani wa asilimia 10.5 ikilinganishwa na asilimia 8.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Mfumuko wa bei usiojumuisha chakula na nishati uliimarika kutoka wastani wa asilimia 2.8 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016 na kuwa asilimia 2.2 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017. Hadi kufikia mwezi Septemba 2017, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 5.3 wakati mfumuko wa bei usiojumuisha bidhaa za chakula na nishati ulikuwa asilimia 1.7.

**Kielelezo Na 1.2: Mwenendo wa Mfumuko wa bei Nchini Tanzania (Januari 2016 - Septemba 2017)**




### (ii) Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

9. Katika kipindi cha mwaka 2016/17, mfumuko wa bei kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki umeendelea kubakia katika kiwango kinachoridhisha cha wastani wa



asilimia 7.7. Kwa kipindi hicho, Tanzania ilikuwa na kiwango cha chini cha mfumuko wa bei cha wastani wa asilimia 5.3 ikifuatiwa na Uganda asilimia 5.7, Rwanda asilimia 7.0, Kenya asilimia 8.1 na Burundi kuwa na kiwango cha juu kati ya nchi zote za Jumuiya cha wastani wa asilimia 12.4 kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.3**. Kwa ujumla kushuka kwa kiwango cha mfumuko wa bei kulisababishwa na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Kielelezo Na 1.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Afrika Mashariki (%)**



### 1.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti 2016/17

10. Katika mwaka 2016/17, utekelezaji wa bajeti ulikuwa wa kuridhisha hususan katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Hata hivyo, kulikuwa na changamoto katika upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na mikopo ya kibiashara kutoka nje. Hali hiyo iliilazimu Serikali kukopa zaidi kutoka vyanzo vya ndani ili kugharamia mahitaji muhimu.

#### 1.3.1 Mapato ya Ndani

11. Katika mwaka 2016/17, Serikali ililenga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 18,463.50. Makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 16,639.8 sawa na asilimia 90.1 ya lengo na ongezeko la asilimia 18.4 ikilinganishwa na makusanyo halisi kwa mwaka 2015/16.

## **Mapato ya Kodi**

12. Katika mwaka 2016/17, Serikali ililenga kukusanya mapato ya kodi ya Shilingi bilioni 15,105.1 sawa na asilimia 13.8 ya Pato la Taifa. Makusanyo halisi yalikuwa Shilingi bilioni 14,126.4 sawa na asilimia 93.5 ya lengo. Licha ya mapungufu ya makusanyo dhidi ya lengo, makusanyo hayo yaliongezeka kwa asilimia 13.2 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2015/16. Aidha, uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa umeongezeka na kufikia asilimia 14.2 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 13.2 mwaka 2015/16. Mafanikio haya yamechangiwa na ufuatiliaji wa karibu wa vyanzo vya mapato, hatua madhubuti na ufuatiliaji makini wa malimbikizo ya kodi, kuongezeka kwa mwitikio wa Taasisi za Serikali katika kukusanya kodi ya zuio wakati wa kufanya malipo kwa bidhaa na huduma mbalimbali.

## **Ufanisi wa Vyanzo Vikuu vya Kodi.**

13. Katika mwaka 2016/17, makusanyo ya kodi ya ushuru wa forodha yalikuwa ni shilingi bilioni 1,538.0 dhidi ya lengo la shilingi bilioni 1,497.6, ikiwa ni ufanisi wa asilimia 2.7 zaidi ya lengo. Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa zisizo za petroli zilizoagizwa nje ya nchi ilikuwa ni shilingi bilioni 1,803.6 dhidi ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 2,102.4. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 85.5 ya lengo na ni ongezeko la asilimia 4.4 ya makusanyo ya mwaka 2015/16. Makusanyo ya kodi ya ushuru wa bidhaa za forodha yalikuwa shilingi bilioni 345.6 sawa na asilimia 62.2 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 555.9. Aidha makusanyo ya ushuru wa bidhaa za forodha yameshuka kwa asilimia 35.9 kutoka shilingi bilioni 539.3 zilizokusanywa mwaka 2015/16. Sababu ya kutokufikiwa kwa malengo ni kupungua kwa thamani ya bidhaa za mlaji (*consumer goods*) ambazo ndio chanzo kikubwa cha kodi hii.

14. Makusanyo ya Kodi zitokanazo na uagizaji wa bidhaa za mafuta yalikuwa ni shilingi bilioni 1,884.8 sawa na asilimia 93.5 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 2,025.8 sawa na ongezeko la asilimia 9.6 ikilinganishwa na makusanyo ya 2015/16. Kodi ya ushuru kwenye bidhaa za petroli, tozo kwenye bidhaa za petroli- REA na tozo kwenye mafuta (fuel) ilikuwa asilimia 97.5, 99.0 na 86.5 ya lengo kwa mtiririko huo. Makusanyo na ukuaji huu ulichangiwa na ufuatiliaji na usimamizi wa karibu wa uagizaji wa bidhaa za petroli.


15. Makusanyo ya kodi za makampuni yalikuwa ni shilingi bilioni 1,450.3 sawa na asilimia 89.8 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 1,615.9 ikiwa ni ongezeko la asilimia 5.1 ikilinganishwa na makusanyo ya 2015/16. Hali hii ilitokana na kushuka kwa mauzo ya bidhaa mabalimbali katika soko la ndani zikiwemo saruji, bia na vinywaji baridi; kupungua kwa kodi ya makampuni kulikosababishwa na makampuni mengi kutopata

faida kama ilivyotarajiwa kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji; na mabenki makubwa kufanya marekebisho ya makisio yao ya kulipa kodi kutokana na kushuka kwa mapato ya riba kufuatia kupungua kwa mikopo.

16. Makusanyo kwenye kodi ya mapato ya ajira yalikuwa shilingi bilioni 2,278.1 sawa na asilimia 90.5 ya lengo la shilingi bilioni 2,516.7 ikiwa ni ongezeko la asilimia 1.4 ikilinganishwa na mwaka 2015/16. Kutofikiwa lengo kwenye kodi za ajira kumetokana na baadhi ya makampuni kupunguza wafanyakazi kufuatia kupungua kwa shughuli za kibiashara. Makampuni hayo ni pamoja na Bulyanhulu, Pangea, Bakhresa Food Products Ltd, SSB Grain Mills Ltd, Azam Bakeries na Kampuni ya Sukari Mtibwa. Vile vile, kupungua kwa ankara za malipo ya mishahara kulikosababishwa na kuahirishwa kwa ajira mpya za Serikali kupisha zoezi la uhakiki wa watumishi wa umma na kufutwa kazi kwa watumishi wa umma waliokosa vigezo vya utumishi kulichangia kupungua kwa kodi ya mapato ya ajira.

17. Kiasi cha kodi kilichokusanywa katika bidhaa na huduma za ndani kilikuwa shilingi bilioni 3,045.5, sawa na asilimia 98 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 3,078.2. Kutofikiwa kwa lengo hususan kwa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa kulisababishwa na kupungua kwa matumizi ya baadhi ya bidhaa za viwandani hususan bia, vinywaji vikali, sigara na vinywaji baridi na hivyo kusababisha makampuni husika kuwasilisha kiasi kidogo cha kodi tofauti na ilivyotarajiwa. Kupungua kwa ukusanyaji wa kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano kulitokana na kuongezeka kwa utoaji wa huduma za mawasiliano kwa vifurushi vya bei nafuu vya muda wa maongezi kulikochangiwa na ushindani wa kibiashara wa kampuni za simu.

**Kielelezo 1.4: Ufanisi wa vyanzo vikuu vya kodi 2015/16- 2016/17**



### **Mapato yasiyo ya Kodi**

18. Katika kipindi cha mwaka 2016/17, makusanyo halisi ya mapato yasiyo ya kodi (bila kujumuisha mapato ya Halmashauri) yalifikia shilingi bilioni 2,072.9, sawa na asilimia 76.3 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 2,718.6. Michango, gawio na marejesho ya mtaji uliozidi kutoka kwenye taasisi na mashirika ya umma ilifikia shilingi bilioni 893.9 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 1,306.54. Makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi yalichangiwa zaidi na ongezeko kubwa la gawio kutoka kwa kampuni na mashirika na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa maduhuli. Mapato yanayokusanywa na Halmashauri yalifikia Shilingi bilioni 511.7, sawa na asilimia 76.0 ya makadirio ya 2016/17.

### **Misamaha ya Kodi**

19. Katika kipindi cha mwaka 2016/17, misamaha ya kodi ilipungua kwa asilimia 14 kutoka Shilingi bilioni 1,103.3 mwaka 2015/16 hadi Shilingi bilioni 952.5. Uwiano wa misamaha ya kodi kwa makusanyo ya kodi ulipungua kutoka asilimia 7.8 mwaka 2015/16 hadi asilimia 6.7. Vile vile, uwiano wa misamaha ya kodi kwa Pato la Taifa ulipungua na kufikia asilimia 0.9 ikilinganishwa na asilimia 1.2 mwaka 2015/16. Kupungua kwa misamaha kumechangiwa na hatua za kisera na za kiutawala zilizochukuliwa na Serikali ambazo zinazolenga kupunguza misamaha isiyo na tija, kuhakiki na kufuatilia misamaha iliyoombwa kabla haijatolewa.

### **1.3.2 Misaada na Mikopo Nafuu kutoka Nje**

20. Katika mwaka 2016/17, Washirika wa Maendeleo waliahidi kutoa Shilingi bilioni 3,600.8 kupitia miradi na programu mbalimbali. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 483.0 zilikuwa Misaada na Mikopo ya Kibajeti, shilingi bilioni 372.1 zilikuwa michango katika Mifuko ya Pamoja ya Kisekta na Shilingi bilioni 2,745.7 zilikuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha zilizopatikana ni asilimia 68.7 ya ahadi. Kati ya kiasi kilichopokelewa, Misaada na Mikopo ya Kibajeti ilikuwa Shilingi bilioni 342.8 sawa na asilimia 71 ya ahadi. Mifuko ya pamoja ya Kisekta ilipata Shilingi bilioni 274.0, sawa na asilimia 73.6 ya ahadi na fedha za maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye miradi zilikuwa Shilingi bilioni 1,857.4, sawa na asilimia 68 ya makisio.

21. Kutofikiwa kwa lengo kwa sehemu kubwa kulitokana na kuairishwa kwa majadiliano kufuatia kutokufikiwa kwa vigezo katika maeneo matatu ambayo ni: nishati na gesi; mazingira ya biashara kwa ajili ya kukuza ajira; na uwazi katika usimamizi wa fedha za umma. Baadhi ya masharti hayo ni pamoja na mapitio ya Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura 290 ili kupunguza kodi za mazao na kutoa msamaha kwa mauzo yasiozidi tani moja ili kuwainua wakulima wadogo na mchango wa Serikali


kwenye miradi hiyo. Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi pia ilichangia kupungua kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa vile utoaji wa fedha za awamu inayofuata hutegemea kukamilika kwa utekelezaji wa awamu iliyotangulia.

**Jedwali Na. 1.3: Mwenendo wa Misaada na mikopo nafuu kutoka nje 2011/12 - 2015/16 (Shilingi Bilioni)**

Mwaka wa Fedha	2012/13		2013/14		2014/15		2015/16		2016/17	
Aina	Bajeti	Halisi	Bajeti	Halisi	Bajeti	Halisi	Bajeti	Halisi	Bajeti	Halisi
Misaada ya Kibajeti	843	919	1,163	1,041	922	717	660	292	483	343
Mifuko ya Pamoja	415	478	500	434	274	290	199	248	372	274
Miradi	1899	1562	2192	1236	1745	1339	1463	1186	2,746	1,857
<b>Jumla</b>	<b>3157</b>	<b>2959</b>	<b>3855</b>	<b>2711</b>	<b>2941</b>	<b>2346</b>	<b>2322</b>	<b>1726</b>	<b>3600.8</b>	<b>2474</b>

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

**Kielelezo 1.5: Mwenendo wa Misaada na mikopo nafuu kutoka nje 2011/12 - 2015/16 (Shilingi Bilioni)**



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

**1.3.3 Matumizi**

22. Bajeti ya mwaka 2016/17 ilikuwa Shilingi bilioni 29,539.6, ambapo shilingi bilioni 17,719.1 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 11,820.5 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2017 kiasi halisi

kilichotolewa ni Shilingi bilioni 23,634.6, sawa na asilimia 80.0 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi cha fedha kilichotolewa kiliongezeka kwa asilimia 6.5 ikilinganisha na shilingi bilioni 22,099.1 zilizotolewa mwaka 2015/16. Kati ya fedha zilizotolewa, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 17,136.2, sawa na asilimia 96.7 na shilingi bilioni 6,498.3 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 55.0 ya makadirio ya mwaka.

23. Sehemu kubwa ya matumizi ya kawaida yalikuwa ni kwaajili ya kugharamia Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS) na mishahara. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali yalikuwa shilingi bilioni 8,781.6 sawa na asilimia 51.2 ya matumizi ya kawaida. Malipo ya mishahara yalikuwa shilingi bilioni 6,367.1 sawa na asilimia 37.2 ya matumizi ya kawaida na asilimia 96.5 ya makadirio ya mwaka.

24. Mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/17 ni pamoja na kugharamia: elimu-msingi bila malipo (Shilingi bilioni 206.9); ununuzi wa ndege mpya mbili (Shilingi bilioni 103.4) na malipo ya awali ya ndege mpya nne (Shilingi bilioni 320.1) kwa ajili ya kuboresha usafiri wa anga; awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (Shilingi bilioni 1,000.0); uwekezaji kwenye miundombinu ya Umeme (Shilingi bilioni 176.5); upanuzi wa miundombinu ya umeme vijijini (Shilingi bilioni 361.5); Ujenzi na ukarabati wa barabara kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara (Shilingi bilioni 807.4); uwekezaji katika miundombinu ya usambazaji maji mijini na vijijini (Shilingi bilioni 137.4); mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu (Shilingi bilioni 495.4); ununuzi wa dawa na vifaa tiba (Shilingi bilioni 165); na upatikanaji wa pembejeo za Kilimo (Shilingi bilioni 21).

25. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na: kupata mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganda hadi Chongoleani-Tanga (dola za Marekani bilioni 3.5) ambapo kupitia mradi huu Taifa litanufaika na ajira, utaalamu na fursa za biashara; upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam (dola za Marekani milioni 345); ununuzi wa asilimia 35 ya hisa za Shirika la Simu Tanzania (TTCL) na kuiwezesha Serikali kumiliki TTCL kwa asilimia 100 (shilingi bilioni 14.9); na kuimarisha ulinzi na usalama wa raia pamoja na ulinzi wa rasilimali za Taifa.

#### **1.3.4 Deni la Taifa**

26. Hadi kufikia June, 2017 Deni la Taifa lilifikia dola za Marekani milioni 26,115.2 ukilinganiasha na dola za Marekani milioni 22,320.76 kwa kipindi kama hicho mwaka 2016, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 17.0. Ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo ili kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo:

*Standard Gauge Railway, Strategic Cities*, mradi wa usafirishaji Dar es Salaam (DART); kuzalisha umeme Malagarasi; na maji safi Dar es Salaam. Kati ya Deni hilo, dola za Marekani milioni 7,643.2 ni deni la ndani na dola za Marekani million 18,472.0 ni deni la nje. Deni la nje linajumuisha deni la Serikali na dhamana ambazo ni dola za Marekani milioni 14,800.5 na deni la sekta binafsi dola za Marekani milioni 3,671.50.

### **Uhimilivu wa Deni la Taifa.**

27. Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134, inaitaka Serikali kufanya uchambuzi wa uhimilivu wa deni kila mwaka ambao pamoja na mambo mengine unaonyesha mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uhimilivu wa deni ikiwa ni pamoja na maelezo ya hali ya Uchumi, katika hali tofauti na kushauri njia za kuimarisha uhimilivu wa deni. Matokeo ya hivi karibuni ya uhimilivu wa Deni la Taifa ya mwezi Novemba 2016 yanaonesha kuwa uwiano wa thamani halisi ya deni la Serikali kwa pato la taifa ni asilimia 32.5. Matokeo hayo yanaonesha kuwa deni la Taifa lipo chini ya ukomo wa hatari na ni himilivu kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Uchambuzi huu umepatikana baada ya kutumia viashiria msingi na vashiria mbadala kwa ajili ya kupima uhimilivu wa deni la Taifa. Viashiria vyote vya athari za madeni vimeendelea kuwa katika wigo unaokubalika kimataifa kama inavyoonekana katika jedwali Na. 1.4.

### **Jedwali 1.4: Viashiria vya Uhimilivu wa Deni**

VIASHIRIA VYA DENI LA NJE	2015/16	2016/17	2017/18	2020/21	2025/26	2035/36	UKOM O
Deni la Nje (PV) / Pato la Taifa	19.9	19	18.8	20.1	18.9	14.2	40
Deni la Nje (PV) / Uuzaji wa Bidhaa Nje	97.7	94.2	98.2	107.4	95.5	71	150
Deni la Nje (PV) / Mapato ya Ndani	145.3	111.46	114.3	98.7	91.8	68.39	250
Ulipaji wa Deni Nje /Uuzaji wa Bidhaa Nje	7.8	9.2	8.4	8	7.9	8	20
Ulipaji wa Deni /Mapato ya Ndani	11.5	11	9.7	7.3	7.6	7.7	20
VIASHIRIA VYA DENI LA NJE NA LA NDANI (Total Debt)							
Deni (PV)/ Pato la Taifa	34.2	32.5	31.2	32.7	29.4	23.3	56
Deni (PV) / Mapato ya Ndani	30.8	21.1	23.4	16.9	16.6	16.1	

Chanzo: WFM - Taarifa ya Uhimilivu wa Deni (DSA) Novemba 2016

## **1.4 Ujazi wa Fedha na Karadha**

### **1.4.1 Ujazi wa Fedha**


28. Mwaka 2016/17, wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikuwa asilimia 6.1 ikilinganishwa na asilimia 12.7 mwaka 2015/16. Mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ambayo ilikua

kwa wastani wa asilimia 1.3 ikilinganishwa na asilimia 19.1 mwaka ulioishia Juni 2016. Katika kipindi hicho, wastani wa ukuaji wa mikopo kwa Serikali Kuu ulipungua kwa asilimia 21 kutoka ukuaji wa asilimia 41.1 kwa mwaka 2015/16. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa amana za Serikali Kuu katika akaunti zake zilizoko Benki Kuu kufuatia kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani, udhibiti wa matumizi na fedha za mikopo kutoka nje.

29. Kasi ndogo ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ilitokana na hatua za tahadhari zilizochukuliwa na benki za biashara katika utoaji mikopo kutokana na ongezeko la mikopo chechefu. Ukuaji wa mikopo uliathiriwa pia na ukuaji mdogo wa amana za sekta binafsi pamoja na uamuzi wa benki kuwekeza zaidi katika dhamana za serikali.

30. Mikopo kwa sekta binafsi kwa mwaka 2016/17, ilipungua katika shughuli kuu za kiuchumi hasa kwenye uchukuzi na mawasiliano, shughuli binafsi pamoja na shughuli za uzalishaji katika kilimo. Mikopo kwa shughuli za viwanda, huduma za kifedha, biashara, hoteli na migahawa iliimarika kidogo, ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli za biashara zikipata wastani wa asilimia 21.6 ya mikopo yote ikifuatiwa na shughuli binafsi zilizokuwa na asilimia 18.8.


**Kielelezo 1.6: Wastani wa Ukuaji wa Mikopo ya Benki kwa Shughuli Kuu za Kiuchumi (Asilimia)**



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



### Kielelezo 1.7: Mchango wa Mikopo ya Benki katika shughuli Kuu za kiuchumi (Asilimia ya Jumla ya Mikopo)




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

#### 1.4.2 Mzunguko wa Sarafu

31. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017, kiasi cha sarafu katika mzunguko kiliongezeka kwa Shilingi bilioni 12.4 ambacho ni cha chini ikilinganishwa na ongezeko la wastani wa Shilingi bilioni 222.6 katika kipindi kama hicho kwa miaka mitatu iliyopita. Ongezeko hili dogo lilitokana na sera ya kupunguza matumizi ya Serikali yasiyo na tija na kupungua kwa kasi ya utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Hata hivyo, kuongezeka kwa huduma za fedha kwa njia ya mtandao kumesaidia kupunguza athari za kupungua kwa mzunguko wa sarafu kwenye ukuaji wa shughuli za kiuchumi.

### Kielelezo 1.8: Mabadiliko ya mzunguko wa sarafu



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### **1.4.3 Mwenendo wa Viwango vya Riba na Udhhibiti wa Ukwasi**

32. Kulingana na hali ya ukwasi katika uchumi, Benki Kuu ilitekeleza sera ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi kupitia zana mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara, kununua fedha za kigeni kutoka kwenye soko la jumla la benki na kushusha riba (discount rate) kutoka asilimia 16.0 hadi asilimia 12.0 kuanzia mwezi Machi 2017; na kupunguza kiwango cha chini cha amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na benki za biashara (Statutory Minimum Reserve Requirement (SMR)) kutoka asilimia 10.0 hadi asilimia 8.0 ya amana za wateja kuanzia mwezi Aprili 2017; na kuruhusu benki hizo kutumia asilimia 10.0 ya sehemu ya SMR bila kuvuka kiwango kinachotakiwa kisheria katika kipindi cha siku kumi na nne. Vile vile, Serikali imeendelea kuwekeza katika miundombinu msingi na kulipa malimbikizo ya madai yaliyohakikiwa kwa lengo la kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi, kuongeza ukwasi kwenye uchumi na kupunguza kiwango cha mikopo chechefu na kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi.


33. Kufuatia hatua hizo, ukwasi kwenye benki uliongezeka na riba ya mikopo baina ya benki (the overnight interbank cash market rate) ilipungua na kufikia asilimia 4.08 kwa Juni 2017 kutoka wastani wa asilimia 14.89 kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2016/17. Vile vile, riba za dhamana za Serikali zilishuka kutoka wastani wa asilimia 15.56 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016/17 hadi kufikia asilimia 7.64 kwa mwezi Juni 2017.

34. Mwenendo wa viwango vya riba katika soko la fedha haukujionesha moja kwa moja katika viwango vya riba kwa benki za biashara. Katika kipindi cha mwaka 2016/17-viwango vya riba za amana vilikuwa vya juu zaidi kuliko mwaka 2015/16. Hali hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa ushindani wa benki katika utafutaji wa amana. Riba za amana ziliongezeka kufikia wastani wa asilimia 9.61 mwaka 2016/17, ikilinganishwa na asilimia 9.25 kwa mwaka 2015/16. Wakati huo huo, riba za amana za kipindi cha mwaka mmoja ziliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 11.66 ikilinganishwa na asilimia 11.17 mwaka 2015/16. Vile vile, viwango vya riba za kukopesha vilikuwa vya juu zaidi ukilinganisha na mwaka uliotangulia kufuatia tahadhari zilizochukuliwa na benki kuepuka kuongezeka kwa mikopo chechefu. Katika kipindi hicho, riba za mikopo ziliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 16.53 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na asilimia 16.17 mwaka 2015/16. Viwango vya riba ya mikopo ya mwaka mmoja ilifikia asilimia 15.38, ikilinganishwa na asilimia 14.19 mwaka 2015/16. Hali hii ilisababisha tofauti kati ya riba ya amana na mikopo ya mwaka mmoja kuongezeka hadi kufikia asilimia 3.72 mwaka 2016/17 kutoka asilimia 3.02 mwaka 2015/16.

#### 1.4.4 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji Fedha

35. Katika kipindi cha mwaka 2016/17, thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani iliendelea kuwa tulivu. Utulivu wa thamani ya shilingi ulitokana na usimamizi na utekelezaji wa sera nzuri ya fedha, usimamizi thabiti wa mapato na matumizi ya Serikali, pamoja na kuimarika kwa urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje. Wastani wa mwenendo wa ubadilishaji Shilingi dhidi ya dola ya Marekani ulikuwa kati ya Shilingi 2,171.0 na Shilingi 2,230.1 kwa dola moja ya Marekani, ikilinganishwa na kati ya Shilingi 2,020.3 na Shilingi 2,182.3 kwa dola moja ya Marekani katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2015/16. Hata hivyo, katikati ya mwezi Januari 2017, thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani iliporomoka kwa kipindi kifupi kutokana na mwenendo wa uchumi wa dunia, hali ambayo baadae ilitengamaa.

#### Kielelezo 1.9: Mwenendo wa thamani ya Shilingi (Shilingi kwa Dola ya Kimarekani)



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

#### 1.4.5 Mwenendo wa Sekta ya Benki

36. Kwa mwaka unaoishia Juni 2017, sekta ya benki imeendelea kuwa imara, salama na yenye kutengeneza faida, ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha. Uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali za benki ulifikia asilimia 18.3 mwezi Juni 2017, ukiwa juu ya kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 10.0, na asilimia 17.2 iliyofikiwa mwezi Juni 2016. Vile vile, uwiano wa rasilimali kwa amana zinazoweza kubadilishwa kwa muda mfupi kuwa fedha taslimu ulifikia asilimia 38.1, ikilinganishwa na kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 20, juu kidogo ya asilimia 37.0 iliyofikiwa mwezi Juni 2016.

37. Thamani ya rasilimali za benki zilitetereka kama inavyojidhirisha katika mikopo chechefu ambayo iliongezeka kufikia asilimia 10.6 kwa mwaka unaoishia Juni 2017 kutoka asilimia 8.9 mwishoni wa mwezi Juni 2016. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Benki Kuu ya Tanzania iliagiza benki zenye uwiano mkubwa wa mikopo chechefu kubuni mikakati ya kushusha uwiano huo kubaki ndani ya kiwango kisichozidi asilimia 5.0. Benki zinahamasishwa pia kuongeza matumizi ya mfumo wa kuhifadhi na kutoa taarifa za wakopaji (*credit reference system*) ili kupunguza mikopo chechefu. Vile vile, faida itokanayo na uwekezaji kwenye rasilimali na mitaji (Return on Assets and equity) ilidorora hivyo kuashiria kupungua kwa mapato na faida. Kwa mwaka ulioishia Juni 2017, faida itokanayo na uwekezaji wa rasilimali ilipungua kufikia asilimia 2.3 wakati faida itokanayo na uwekezaji wa mitaji ilipungua kufikia asilimia 10.4 ikilinganishwa na asilimia 3.0 na asilimia 15.3 kwa mtiririko huo, katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

### Jedwali 1.5: Mwenendo wa Viashiria vya sekta ya Benki (Asilimia)

Kiashiria	Ukomo Kisheria	Jun-16	Sep-16	Des-16	Mach-17	Jun-17
Utoshlevu wa mtaji						
Uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali za benki	Kiwango cha chini 10	17.2	17.3	17.8	19.0	18.3
Uwiano wa mtaji wote kwa rasilimali za benki	Kiwango cha chini 12	19.2	19.2	19.8	21.0	20.3
Ukwasi						
Uwiano wa rasilimali zenye ukwasi kwa amana zinazoweza kuhitajika kwa muda mfupi	Kiwango cha chini 20	37.0	34.2	42.4	36.0	38.1
Uwiano wa mikopo kwa amana za wateja		85.8	87.1	86.3	86.0	83.1
Mapato na faida						
Faida kutokana na uwekezaji wa rasilimali		3.0	2.5	2.4	2.4	2.3
Faida kutokana na uwekezaji wa mtaji		15.3	12.0	10.5	11.3	10.4
Uwiano wa matumizi usiojumisha malipo ya riba kwa mapato yote		65.0	66.9	67.6	67.3	51.5
Ubora wa Rasilimali						
Uwiano wa mikopo chechefu kwa mikopo yote		8.9	9.1	9.5	11.0	10.6

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### 1.5 Mwenendo wa Sekta ya Nje

38. Nakisi katika urari wa malipo ya kawaida ilipungua kutoka dola za Marekani milioni 2,954 mwaka 2015/16 hadi dola za Marekani milioni 1,350 mwaka 2016/17 kutokana na upungufu mkubwa wa thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma na kushuka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida kwa mwaka 2016/17 ilikuwa asilimia 2.8 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2015/16. Kufuatia mwenendo huo, urari wa malipo yote ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,226 kutoka nakisi ya dola za Marekani milioni 368 kwa mwaka ulioishia Juni 2016. Vile vile, akiba ya fedha za kigeni mwishoni mwa mwezi Juni 2017 ilifikia dola za Marekani milioni 5,022 zinazotosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 5.8 bila kuhusisha

bidhaa zinazotokana na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje.

39. Mwaka 2016/17, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilipungua kidogo kwa asilimia 0.8 kufikia dola za Marekani milioni 8,908.0 ikilinganishwa na dola za marekani milioni 8,981.0 mwaka 2015/16 ikichagizwa zaidi na kupungua kwa mauzo ya bidhaa za viwandani nje. Mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi yalipungua kwa asilimia 29.8 kufikia dola za Marekani milioni 893.0 kutoka dola za Marekani milioni 1,273 mwaka 2015/16. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wasiwasi wa kiusalama katika nchi jirani hususan DRC, ambayo ni miongoni mwa soko kubwa la bidhaa za viwandani zinazozalishwa nchini. Hata hivyo, maeneo yaliyofanya vizuri ni pamoja na mapato yatokanayo na huduma za usafirishaji, mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia. Thamani ya mauzo ya dhahabu nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,517.9 kutoka dola za Marekani milioni 1,243.3, kutokana na kuongezeka kwa kiasi cha dhahabu zilizouzwa na bei yake katika soko la dunia.

### Jedwali Na 1.6: Urari wa Malipo ya Kawaida

	<i>Dola za Marekani Milioni</i>		
	<b>2015/16</b>	<b>2016/17<sup>P</sup></b>	<b>Badiliko %</b>
<b>Bidhaa</b>	<b>-3,333.4</b>	<b>-2,327.1</b>	<b>-30.2</b>
Mauzo nje	5,584.6	5,238.3	-6.2
Uagizaji nje	8,918.0	7,565.4	-15.2
<b>Huduma</b>	<b>887.5</b>	<b>1,639.3</b>	<b>84.7</b>
Mapato	3,396.2	3,669.6	8.1
Malipo	2,508.7	2,030.3	-19.1
<b>Bidhaa na Huduma</b>	<b>-2,445.9</b>	<b>-687.9</b>	<b>-71.9</b>
Mauzo ya bidhaa na huduma	8,980.8	8,907.9	-0.8
Uagizaji wa bidhaa na huduma	11,426.7	9,595.7	-16.0
<b>Mapato ya Vitega Uchumi</b>	<b>-840.9</b>	<b>-1,099.6</b>	<b>30.8</b>
Mapato	100.8	105.7	4.9
Malipo	941.7	1,205.3	28.0
<b>Uhamisho wa Mali</b>	<b>332.5</b>	<b>437.7</b>	<b>31.6</b>
Zilizoingia	410.5	502.7	22.5
Kwa Serikali Kuu	40.8	140.2	243.6
Zilizotoka	78.0	65.0	-16.7
<b>Urari wa Malipo ya Kawaida</b>	<b>-2,954.3</b>	<b>-1,349.8</b>	<b>-54.3</b>

*P= halisi za awali*

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

40. Katika mwaka 2016/17, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 9,595.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni

11,426.7 mwaka 2015/16. Upungufu huo ulionekana zaidi katika uagizaji wa bidhaa za ukuzaji mitaji, mafuta ya petroli na chakula. Thamani ya mafuta yaliyoagizwa, ambayo huchangia sehemu kubwa ya bidhaa zinazoagizwa ilipungua kwa asilimia 8.5 kufikia dola za Marekani milioni 2,803.2 kutokana na kushuka kwa bei katika soko la dunia wakati kiasi cha mafuta kilichoagizwa kiliongezeka. Kupungua kwa uagizaji pia kulitokana na kuwepo kwa hali nzuri ya utoshelevu wa chakula nchini na kukamilika kwa miradi mikubwa ikiwemo ujenzi wa kiwanda cha saruji cha Dangote, ujenzi wa bomba la gesi na ujenzi wa mitambo ya kufua umeme wa Kinyerezi I.

## **1.6 Mwelekeo wa Uchumi na Maoteo ya Muda wa Kati**

### **1.6.1 Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia**

41. Kwa mujibu wa taarifa ya mwelekeo wa uchumi wa Dunia ya Shirika la Fedha la Kimataifa, ya Oktoba 2017, uchumi wa Dunia unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.6 mwaka 2017 na asilimia 3.7 mwaka 2018. Maoteo haya ni kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika Nchi Zilizoendela na Nchi Zinazoibukia Kiuchumi kwa mwaka 2017.

42. Uchumi wa Nchi Zilizoendela unatarajiwa kukua kwa asilimia 2.2 mwaka 2017 na asilimia 2.0 mwaka 2018. Maoteo ya ukuaji wa uchumi wa Marekani ni asilimia 2.2 mwaka 2017 na asilimia 2.3 mwaka 2018. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi ya Uingereza inatarajiwa kupungua kutoka asilimia 1.8 mwaka 2016 hadi asilimia 1.7 mwaka 2017 kutokana na kupungua kwa ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi katika robo ya kwanza ya mwaka 2017. Ukuaji huo unatarajiwa kuendelea kupungua zaidi kufikia asilimia 1.5 mwaka 2018.

43. Nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi zinatarajiwa kushuhudia kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, ambapo kasi ya ukuaji wa uchumi itaimarika kutoka asilimia 4.3 mwaka 2016 kufika asilimia 4.6 mwaka 2017 na asilimia 4.9 mwaka 2018. Maoteo hayo ya ukuaji wa uchumi yanatokana na kuimarika kwa uchumi wa nchi zinazouza nje bidhaa za viwandani zilizokumbwa na mdororo mwaka 2015/16. Uchumi wa China unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.8 mwaka 2017 na kupungua kidogo kufikia wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2018. Uchumi wa India unatarajiwa kuimarika kufikia ukuaji wa asilimia 6.7 na asilimia 7.4 mwaka 2017 na mwaka 2018 kwa mtiririko huo, kutokana na kuimarika kwa matumizi ya serikali na mapitio ya takwimu yaliyoashiria kuimarika kwa uchumi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017.

44. Katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 2.6 mwaka 2017 ikiwa ni juu kidogo ya maoteo ya awali kutokana na kuimarika kwa maoteo ya ukuaji wa uchumi wa nchi ya Afrika Kusini, kufuatia mavuno mengi ya kilimo yaliyotokana na hali nzuri ya mvua na kuimarika kwa shughuli za uchimbaji wa madini. Uchumi wa nchi hizo unatarajiwa kuendelea kuimarika kufikia ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2018.

### Jedwali Na. 1.7: Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Maoteo (%)

	Halisi			Maoteo	
	2014	2015	2016	2017	2018
Dunia	3.6	3.4	3.2	3.6	3.7
Nchi zilizoendelea	2.1	2.2	1.7	2.2	2.0
Nchi zinazoendelea	4.7	4.3	4.3	4.6	4.9
Nchi zinazoendelea za Asia	6.8	6.8	6.4	6.5	6.5
China	7.3	6.9	6.7	6.8	6.5
India	7.2	8.0	7.1	6.7	7.4
Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara	5.1	3.4	1.3	2.6	3.4
Tanzania	7.0	7.0	7.0	7.0	7.1
Kenya	5.4	5.7	5.8	5.0	5.5
Uganda	4.6	5.7	2.3	4.4	5.2
Rwanda	7.6	8.9	5.9	6.2	6.8
Burundi	4.5	-4.0	-1.0	0.0	0.1

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa Oktoba, 2017

### Misingi ya Uchumi Jumla

45. Ili kufikia malengo ya ukuaji wa uchumi, ipo Misingi mbalimbali iliyobaoinishwa na kuzingatiwa wakati wa kuweka malengo husika. Baadhi ya Misingi iliyozingatiwa katika kuweka malengo ya uchumi jumla na kisera katika kipindi cha muda wa kati (2018/19-2020/21) ni pamoja na:

- i. Kuendelea kuimarishwa na kudumishwa kwa amani, usalama, utulivu na umoja wa ndani na nchi jirani;
- ii. Kuimarika kwa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama vile Pato la Taifa, ukusanyaji wa mapato ya ndani na mfumuko wa bei;
- iii. Kuendelea kuimarika na kutengemaa kwa uchumi wa dunia;
- iv. Kuendela kuwa na utulivu wa bei za mafuta katika soko la dunia; na
- v. Hali ya hewa nzuri ndani ya nchi na katika nchi jirani.

## **Ukuaji wa Uchumi**

46. Makadirio ya ukuaji wa Pato la Taifa yamezingatia chambuzi wa viashiria mbalimbali katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017. Uchambuzi wa hivi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 unaonesha yafuatayo:

- i. Pato la Taifa katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 lilikua kwa asilimia 6.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.7 ulioshuhudiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016;
- ii. Uzalishaji wa saruji uliongezeka kufikia tani 2,220,400 ikilinganishwa na tani 1,953,800 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 13.6. Uzalishaji wa saruji hutumika sio tu kama sehemu ya uzalishaji wa bidhaa za viwandani, bali pia kama sehemu ya shughuli za kiuchumi za ujenzi;
- iii. Uzalishaji wa umeme katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 uliongezeka kufikia kWh milioni 3,476.1 ikilinganishwa na kWh milioni 3,454.2 mwaka 2016, kutokana na vyanzo vya maji na gesi asilia. Umeme ni nyenzo muhimu kwa sekta mbalimbali zikiwemo uzalishaji viwandani na biashara;
- iv. Mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi yalipungua kwa asilimia 24.6 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 na kufikia Dola za Marekani milioni 481.3 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2016;
- v. Vyanzo mbalimbali vya mapato ya kodi vimeonesha ukuaji mzuri isipokuwa kwa ushuru wa forodha. Hata hivyo, makundi makuu ya ushuru wa bidhaa yalikuwa na ukuaji mdogo katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2016 kutokana na kupungua kwa shughuli za uzalishaji na za mlaji;
- vi. Katika kipindi cha mwaka unaoishia Juni 2017, mikopo ya benki kwa sekta binafsi ilikuwa kwa asilimia 1.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 19.1 ulioshuhudiwa katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2016. Kupungua kwa ukuaji wa mikopo ya benki kwa sekta binafsi kunaweza kupunguza kiwango cha uwekezaji wa sekta binafsi na biashara, hivyo kuathiri ukuaji wa Pato la Taifa; na
- vii. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017, ujazi wa fedha kwa tafsi pana (M3) uliongezeka kwa Shilingi bilioni 12.4, kiwango ambacho ni kidogo ikilinganishwa na wastani wa Shilingi bilioni 222.6 kilichoshuhudiwa katika kipindi kama hicho kwa miaka mitatu iliyopita.


47. Kama inavyojidhihirisha, viashiria vingi vya ukuaji wa uchumi havikufikia malengo tarajiwa katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017. Hivyo, maoteo ya ukuaji wa Pato la Taifa kwa mwaka 2017 yamefanyiwa mapitio na kupunguzwa kutoka maoteo ya awali ya asilimia 7.1 hadi asilimia 7.0. Hata hivyo, inatarajiwa kuwa utekelezaji mzuri wa Sera



za Serikali, ikijumuisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21, utaimarisha kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa, kufikia wastani wa asilimia 7.4 katika kipindi cha muda wa kati.

48. Maoteo ya ukuaji wa muda wa kati yanatokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali katika miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini hususan katika vyanzo vya maji (mradi wa Stigler’s Gorge) na gesi asilia (miradi ya Kinyerezi I hadi IV) inayotarajiwa kuinua ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi ikiwemo uzalishaji viwandani na biashara; ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*; kufufua na kuboresha utendaji wa Shirika la Ndege Tanzania kwa kununua ndege mpya; kuendeleza maeneo maalum ya kiuchumi; ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); mradi wa shamba la miwa na kiwanda cha sukari Mkulazi na Mbigiri - Morogoro; makaa ya mawe – Mchuchuma na chuma – Liganga; Mtambo wa kuchakata gesi kimiminika - Lindi; kuongeza uwezo na ufanisi wa bandari za Dar es Salaam, Tanga, na Mtwara; kuongezeka kwa shughuli za utafiti na uzalishaji wa gesi asilia; na kuendelea kuimarika kwa huduma za kifedha katika maeneo yote nchini.

**Kielelezo Na. 1.10: Ukuaji Halisi wa Uchumi na Maoteo (2008/09-2020/21)**



Angalizo: Mwaka wa Kalenda, mfano 2008/09 ni 2009.

## Jedwali Na. 1.8: Pato la Taifa (Halisi na Maoteo)

PATO LA TAIFA KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA (SHILINGI BIL.)								
2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
70,953.2	79,718.4	90,863.8	103,744.6	110,013.1	127,625.7	138,131.2	156,931.7	174,626.8
PATO HALISI LA TAIFA (SHILINGI BIL.)								
2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
38,546.5	41,231.4	44,100.8	47,174.9	50,454.2	54,022.2	57,987.5	62,392.9	67,356.7
PATO LA TAIFA KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA (SHILINGI BIL.)								
2012/13	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
66,193.7	75,335.8	85,291.1	97,304.2	106,878.9	118,819.4	132,878.4	147,531.5	165,779.2
PATO HALISI LA TAIFA (SHILINGI BIL.)								
2012/13	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
37,241.5	39,889.0	42,666.1	45,637.9	48,814.5	52,238.2	56,004.8	60,190.2	64,874.8

*Chanzo: Imetolewa kutoka FP Agosti, 2017*

### Makadirio ya Mfumuko wa Bei

49. Mfumuko wa bei unakadiriwa kubaki katika kiwango cha tarakimu moja cha wastani wa asilimia 5.0 ifikapo Juni 2018, na kuendelea kubaki katika wastani huo katika kipindi cha muda wa kati. Makadirio haya ya mfumuko wa bei yanatokana na sababu zifuatazo:

- i. Kupungua kwa gharama za uzalishaji kutokana na kuimarika kwa uzalishaji, usafirishaji na usamabazaji wa umeme na kwa bei nafuu pamoja na kupungua kwa gharama za uagizaji wa mafuta mazito kwa ajili ya uzalishaji wa umeme;
- ii. Kuimarika kwa upatikanaji wa chakula nchini katika msimu wa mwaka 2017/18 kutokana na hali ya hewa nzuri nchini. Taarifa ya *Famine Early Warning System Network* (FEWSNET) ya Agosti 2017 inaonesha kuwa uzalishaji wa nafaka nchini unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 14 ikilinganishwa na uzalishaji wa mwaka jana;
- iii. Kupungua kwa athari za ongezeko la bei ya nishati ya mafuta katika soko la dunia kutokana na matumizi ya gesi asilia kama chanzo mbadala cha uzalishaji wa nishati ya umeme; na
- iv. Sera imara za fedha ikijumuisha sera za usimamizi wa matumizi.

## **Sera za Fedha**

50. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) unatarajiwa kuendelea kukua sanjari na ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuimarika kwa mzunguko wa fedha. Ukuaji wa M3 unatarajia kuimarika kufikia asilimia 12.0 Juni 2018 kutoka ukuaji wa asilimia 6.1 ulioshuhudiwa Juni 2017, wakati huo mikopo ya benki kwa sekta binafsi inakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 10 kutoka asilimia 1.3. Katika kipindi cha muda wa kati, ukuaji wa M3 unatarajiwa kuwa katika kiwango cha asilimia 12.5, wakati mikopo ya benki kwa sekta binafsi itakua kwa wastani wa asilimi 18.

## **Biashara za Nje**

51. Urari wa malipo ya kawaida unatarajiwa kuwa na nakisi ya asilimia 4.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2017/18 ikilinganishwa na nakisi ya asilimia 2.8 katika mwaka uliotangulia. Katika kipindi cha muda wa kati, urari wa malipo ya kawaida unatarajiwa kuwa na nakisi ya wastani wa asilimia 6.6 ya Pato la Taifa kutokana na ongezeko kubwa la uagizaji wa bidhaa za mtaji kwa ajili ya ujenzi wa viwanda ikilinganishwa na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

52. Mauzo ya bidhaa na huduma nje kwa mwaka 2017/18 yanatarajiwa kufikia asilimia 17.6 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na asilimia 18.3 kwa mwaka 2016/17. Katika kipindi cha muda wa kati, mauzo ya bidhaa na huduma nje yanatarajiwa kuwa wastani wa asilimia 16.4 ya Pato la Taifa.

53. Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi unakadiriwa kufikia asilimia 21.4 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 19.7 kwa mwaka uliotangulia. Ongezeko hili la uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi ni kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kama vile utekelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji ikijumuisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, mradi wa kuzalisha umeme wa Stigler's Gorge na ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga. Katika kipindi cha muda wa kati uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi unatarajiwa kuwa wa wastani wa asilimia 22.6 ya Pato la Taifa.

## **SURA YA PILI**

### **MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2018/19 - 2020/21**

#### **2.1 Utangulizi**

54. Sura hii inaainisha maeneo muhimu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha muda wa kati kama ilivyoainishwa na Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015, pamoja na Kanuni za bajeti zake. Sheria ya Bajeti inaelekeza umuhimu wa kuzingatia usimamizi endelevu wa fedha za umma na kuhakikisha kuwa viwango vya mapato na matumizi kama vilivyowasilishwa katika Bajeti pamoja na miaka miwili inayofuatia vimejengwa katika misingi imara na thabiti ya mfumo wa uchumi jumla.

55. Mgawanyo wa mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/19 pamoja na miaka miwili inayofuatia inatoa picha kamili ya utekelezaji na usimamizi wa fedha za umma katika kuhakikisha malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/19) yanatekelezwa kwa ufanisi. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeandaa Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kulingana na mahitaji ya rasilimali fedha katika kutekeleza Mpango; lengo ni kuwa na rasilimali fedha za kutosha ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kupunguza athari za Mpango kutotekelezeka.

56. Mkakati umeainisha upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka katika vyanzo vya kawaida (traditional sources) vinavyojumuisha mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi, mikopo ya ndani na mikopo ya nje; Ikiwa ni pamoja na kuainisha vyanzo bunifu vya upatikanaji wa rasilimali fedha kwa kutumia Hati Fungani kwa Serikali za Mitaa, Mifuko ya Fedha za Pensheni, Hati Fungani kwa Masoko ya fedha ya kimataifa, Mfuko wa Fedha za Mazingira, Ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi; na uimarishaji wa matumizi ya Taasisi za Fedha na Benki za maendeleo katika kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

57. Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19, inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 32,476.0 ambayo ni ongezeko la asilimia 2.4 ya bajeti ya mwaka 2017/18 yenye jumla shilingi bilioni 31,712.0 kama ilivyopitishwa na Bunge. Sura ya Bajeti ya Serikali kwa muda wa kati (2018/19 hadi 2020/21) imeoneshwa katika Jedwali Na. 2.1. Viwango hivi vya awali vya mgawanyo wa mapato na matumizi vinaashiria jinsi Serikali ilivyojikita katika kutekeleza sera na malengo ya muda wa kati.

## **2.2 Sera za Kibajeti**

### **2.2.1 Sera za Mapato**

58. Serikali itaendelea kuimarisha na kujenga misingi na mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kuwa na mapato endelevu kwa ajili ya kugharamia matumizi yake. Usimamizi madhubuti wa ukusanyaji wa mapato utasaidia kupanua wigo na kudhibiti ukwepaji wa kodi kupitia urasimishaji wa shughuli za uchumi kwa kuwezesha ukuaji wa biashara katika sekta ndogo na za kati ambazo ndiyo muhimili wa kuzalisha ajira na kukuza uchumi.

59. Katika kipindi cha muda wa kati, utekelezaji wa hatua za kisera na usimamizi wa mapato unatarajiwa kuongeza mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Serikali za Mitaa inakadiriwa kuwa asilimia 16.6 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19. Uwiano huu wa mapato ya ndani na Pato la Taifa unaendana na wastani wa nchi za kipato cha chini zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

### **Mapato ya Kodi**

60. Serikali itaendelea kusimamia dhana ya kulipa kodi kwa hiari kwa kuimarisha Mkakati Shirikishi wa Mawasiliano na Walipa kodi na kuboresha utaratibu wa utozaji kodi ya mapato kwa wafanyabiashara wadogo 'presumptive taxation scheme'. Hatua za kiutawala zitakazochukuliwa ni pamoja na; kuwa na kituo kimoja cha kushughulikia nyaraka za mizigo forodhani kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Dirisha Moja kwa watoa huduma na wadau wa bandari na vituo vya forodha vya mipakani; kuhuisha mifumo ya kielektroniki ya taarifa za kodi; kuimarisha udhibiti na usimamizi wa Bandari ya Dar es Salaam na vituo vingine vya forodha; na kuendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa walipa kodi kwenye kanzidata.

61. Aidha, Serikali itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ili kukabiliana na tatizo la uhamishaji faida (Transfer Pricing) unaofanywa na makampuni yenye mitandao ya kimataifa kwa lengo la kukwepa au kupunguza kodi; kuboresha ridhaa ya ulipaji kodi kwa kuzingatia viashiria hatarishi vya uvujaji wa mapato; kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa ulipaji kodi kupitia Mfumo wa Vitalu vya Walipakodi; na kuimarisha ubadilishanaji wa taarifa na taasisi za Serikali pamoja na Mamlaka za Mapato za Kikanda ili kupambana na tatizo la ukwepaji kodi.

62. Hatua za sera na usimamizi wa kodi zitalenga kukuza uwiano wa mapato ya kodi kuwa asilimia 14.2 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19.

## **Mapato yasiyo ya Kodi**

63. Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kisera na kiusimamizi ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza hatua kwa hatua mpango wa kuhamisha majukumu ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato (*Government e-Payment Revenue Gateway System*) ili uweze kutumika katika utoaji wa taarifa za makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi. Vile vile, Serikali itaendelea kuhimiza uhamishaji wa mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma kwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

64. Serikali itaendelea na juhudi za kuongeza mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma hadi kufikia asilimia 1.9 ya Pato la Taifa kwa muda wa kipindi cha kati.

65. Hatua mahsusi za kisera na kiusimamizi kwa ajili ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ni pamoja na;

- (i) Kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipakodi wapya kwa mujibu wa sheria hususan Kodi ya Mapato, na Kodi ya Ongezeko la Thamani;
- (ii) Kutekeleza matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Stempu za Kodi kwa ajili ya kupunguza ukwepaji kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi, bia na sigara;
- (iii) Ufuatiliaji wa mara kwa mara wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki (EFD) na utekelezaji wa vivutio vya kodi kwa lengo la kudhibiti upotevu wa mapato;
- (iv) Kuendelea kupitia ada, tozo na kodi zinazotozwa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Mamlaka za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma;
- (v) Kuendelea kuhimiza matumizi ya Mfumo wa Serikali wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato;
- (vi) Kuendelea kuhimiza ufuatiliaji kwa Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuhakikisha gawio, michango na ziada stahiki zinawasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali;
- (vii) Kuendelea kufanya uthamini wa mkupuo wa majengo na kusimamia ulipaji ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya majengo;

- (viii) Kuendelea kurasimisha miliki za ardhi kwa lengo la kuongeza mapato; na
- (ix) Kuendelea kupitia viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ili kuendana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi.

### **Misaada na Mikopo**

66. Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa pamoja wamekubaliana juu ya Mfumo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Cooperation Framework) ulioboreshwa ambao utanza kutumika katika mwaka wa fedha 2018/19. Mfumo huu utawezesha Washirika wa Maendeleo kutimiza ahadi na kuleta ufanisi katika kutekeleza bajeti ya Serikali.

67. Katika kipindi cha muda wa kati, misaada ya Washirika wa Maendeleo itaendelea kuwa chanzo muhimu katika kugharamia bajeti ya Serikali. Hata hivyo, Serikali itaendelea na juhudi za kukusanya mapato ili kupunguza utegemezi wa misaada na kufikia malengo ya maendeleo iliyojiwekea.

68. Makadirio ya bajeti ya mwaka 2018/19, yanaonesha Washirika wa Maendeleo watachangia kiasi cha shilingi bilioni 3,658.2, ambapo misaada ya kibajeti ni shilingi bilioni 946.0, mifuko ya kisekta ni shilingi bilioni 558.9 na miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 2,153.3.

### **2.2.2 Sera za Matumizi**

69. Umakini katika kupanga matumizi na nidhamu ya usimamizi wa fedha za umma ndizo nguzo kuu za utengemavu wa utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha muda wa kati. Sera ya matumizi katika kipindi cha muda wa kati zimeleza kulinda mafanikio yaliyotokana na kuwa na sera thabiti za kibajeti na utengemavu wa uchumi. Aidha, zimeleza pia kutimiza dhamira ya serikali ya kufuata itifaki ya Umoja wa Kifedha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sera ya matumizi inalenga kupunguza matumizi ya kawaida katika bajeti ya Serikali ili kupata fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya miundombinu.

70. Katika kipindi cha muda wa kati fedha za maendeleo zitaendelea kutengwa katika kiwango cha asilimia 30 hadi 40 ya bajeti ya Serikali. Lengo ni kutekeleza miradi ya kimkakati (Miradi ya vielelezo) na miradi mingine muhimu. Miradi ya kibiashara inayovutia kwa sekta binafsi itagharamiwa kwa utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi. Serikali itaendelea kugharamia matumizi ya maendeleo yenye vyanzo mahsusi kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo maalum yenye maslahi mapana kwa Taifa kama vile Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Reli, Mfuko wa Umeme Vijijini na Mfuko wa Maji.

71. Matumizi ya Serikali katika mwaka 2018/19 yanakadiriwa kuwa jumla ya shilingi bilioni 32,476.0 sawa na asilimia 24.5 ya Pato la Taifa. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 20,227.6 sawa na asilimia 15.2 ya Pato la Taifa ambapo mishahara (ikijumuisha mishahara ya mashirika) inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 7,627.7 (asilimia 5.7 ya Pato la Taifa) na Huduma za Mfuko wa Hazina (CFS) zinatarajiwa kuwa shilingi bilioni 9,705.2 (asilimia 7.3 ya Pato la Taifa). Matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 12,248.3 sawa na asilimia 9.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2018/19.

### **2.2.3 Usimamizi wa Malimbikizo ya Madeni**

72. Serikali inaendelea na msimamo wa kisera ulioainishwa katika Waraka wa Hazina Na 4 wa Mwaka 2014/15 unaotoa maelekezo na mikakati yenye kuboresha utekelezaji wa Bajeti hususan kupunguza malimbikizo na kuzuia uzalishaji wa madeni mapya ya ndani. Serikali imeendelea kuweka msisitizo katika kusimamia matumizi ya fedha za umma na kuzitaka Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma kuandaa na kuwasilisha mipango kazi na mtiririko wa fedha iliyozingatia vipaumbele vya bajeti ili iweze kutumika katika ugawaji wa rasilimali fedha.

73. Serikali itaendelea kuhakiki madai na kulipa kwa awamu kwa kutumia fedha zilizotengwa mahsusi kwa ajili ya kupunguza malimbikizo ya Madeni ya Wakandarasi, Watoa huduma na Watumishi wa umma katika bajeti ya serikali. Mikakati mingine ni pamoja na:

- (i) Kuchambua Mfumo wa Bajeti wa muda wa kati (MTEF) kwa Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma ili kuhakikisha upangaji makini wa matumizi wenye kuzingatia vipaumbele ili kuepuka matumizi yasiyo ya lazima;
- (ii) Kuzuia utoaji wa huduma na bidhaa kwa Serikali zisizokuwa na hati ya manunuzi (LPO) kutoka kwenye Mfumo wa malipo (IFMIS);
- (iii) Kuhakikisha kwamba mihadi yote ya huduma na uingiaji mikataba kwa Serikali inaambatana na kuwepo kwa hati ya matumizi; na
- (iv) Taasisi za Serikali kupata kibali cha kukopa kutoka kwa Waziri wa Fedha na Mipango kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada kwa Serikali, SURA 134;
- (v) Kufanya ununuzi kupitia taasisi za serikali zilizopo ili kupunguza gharama; kwa mfano ununuzi wa magari katika sekta ya umma yafanywe na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini.



#### **2.2.4 Sera za Kugharamia Nakisi ya Bajeti**

74. Serikali itaendelea kutumia mikopo kutoka katika vyanzo vya ndani na nje kugharamia nakisi ya bajeti. Kiasi kikubwa cha mikopo kutoka vyanzo vya nje itakuwa yenye masharti nafuu ambapo mikopo yenye masharti ya kibiashara itakopwa kwa uangalifu na kutumika kugharamia miradi ya maendeleo inayolipa. Serikali itaendelea kutumia zaidi mikopo kutoka kwenye Taasisi za Fedha za Kimataifa na Wakala wa Mikopo (Export Credit Agencies) yenye masharti nafuu kugharamia miradi ya maendeleo ikilinganishwa na wakopeshaji wengine kama ilivyoainishwa kwenye Mkakati wa kipindi cha Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Taifa wa mwaka 2016. Aidha, kukamilika kwa zoezi la tathmini ya uwezo wa nchi wa kukopa na kulipa madeni, kutaiwezesha Serikali kuuza hatifungani katika soko la fedha la kimataifa (Euro Bond) hatua ambayo itaongeza vyanzo vya ukopaji na hivyo kupunguza utegemezi katika soko la fedha la ndani.

75. Serikali itaendelea kukopa katika soko la ndani kwa kiwango ambacho hakitaathiri utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Vile vile, Serikali imedhamiria kuongeza wastani wa muda wa uivaji wa madeni ya ndani ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza za kutumia utaratibu wa kukopa kurejesha mikopo iliyoiva 'rollover'. Kwa upande wa mikopo ya nje, Serikali itaendelea kukopa zaidi mikopo yenye viwango vya riba visivyobadilika ili kupunguza athari za mabadiliko ya viwango vya riba.

76. Kwa kuzingatia makadirio ya mapato na matumizi, katika mwaka 2018/19 nakisi ya bajeti bila misaada, inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 4,612.4 (sawa na asilimia 3.5 ya Pato la Taifa) ikilinganishwa na makadirio ya nakisi ya bajeti ya shilingi bilioni 5,604.1 (sawa na asilimia 4.6 ya Pato la taifa) mwaka 2017/18. Katika mwaka 2018/19 nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 3,310.5 sawa na asilimia 2.5 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na makadirio ya nakisi ya bajeti ya shilingi bilioni 4,560.3 sawa na asilimia 3.8 ya pato la taifa kwa mwaka 2017/18. Nakisi ya Bajeti ya mwaka 2018/19 ambayo ni asilimia 2.5 ya Pato la Taifa, itagharamiwa kwa kukopa shilingi bilioni 1,983.5 kutoka vyanzo vya nje ambayo ni sawa na asilimia 1.5 ya Pato la Taifa na Shilingi bilioni 1,327.0 sawa na asilimia 1 ya Pato la Taifa kutoka vyanzo vya ndani.

## Jedwali Na. 2.1: Mfumo wa Bajeti kwa Mwaka 2016/17-2020/21 (Shilingi milioni)

	2016/17 APPROVED BUDGET	2016/17 ACTUAL BUDGET	2017/18 APPROVED BUDGET	2018/19 PROJECTED BUDGET	2019/20 PROJECTED BUDGET	2020/21 PROJECTED BUDGET
<b>I. TOTAL RESOURCES</b>	<b>29,539,603</b>	<b>23,634,550</b>	<b>31,711,986</b>	<b>32,475,950</b>	<b>35,429,541</b>	<b>39,066,057</b>
<b>Domestic Revenue including LGAs own source</b>	18,463,532	16,639,831	19,977,001	22,088,150	24,885,709	28,251,708
Domestic revenue	17,798,118	16,128,113	19,289,695	21,240,498	23,953,292	27,226,050
Tax Revenue (TRA)	15,105,100	14,126,488	17,106,336	18,816,970	21,263,176	24,240,020
O/w Non Tax Revenue	2,693,018	2,001,625	2,183,359	2,423,528	2,690,117	2,986,029
LGAs Own Sources	665,415	511,718	687,306	847,652	932,417	1,025,659
Programme loan and grants	483,002	342,785	941,258	945,986	962,840	979,984
Project loans and grants	2,745,659	1,857,399	2,473,770	2,153,312	2,150,918	2,189,215
Basket Support Loans	193,472	104,991	355,454	357,239	363,604	370,078
Basket Support Grants	178,675	168,984	200,621	201,629	205,222	208,876
Domestic Borrowing (Rollover)	3,777,112	4,615,670	4,948,229	4,028,593	3,990,300	3,990,300
Net Domestic Financing	1,597,157	-110,862	1,220,668	1,327,040	1,472,467	1,652,516
Adjustment to cash	0	0	0	0	0	0
Non-Concessional borrowing	2,100,995	1,226,760	1,594,985	1,374,000	1,398,480	1,423,380
Financing Gap	0	-1,211,008	0	0	0	0
<b>II. TOTAL EXPENDITURE</b>	<b>29,539,603</b>	<b>23,634,550</b>	<b>31,711,986</b>	<b>32,475,950</b>	<b>35,429,541</b>	<b>39,066,057</b>
<b>RECURRENT EXPENDITURE</b>	17,719,100	17,136,246	19,712,394	20,227,617	23,300,437	24,732,170
CFS	8,000,000	8,781,628	9,461,433	9,705,237	11,137,342	11,299,678
o/w Interest payments	1,709,922	1,715,429	1,699,038	2,208,015	2,847,465	3,059,367
Pension Bond	0	0	50,000	0	0	0
Amortization	4,742,980	5,519,101	6,130,880	5,775,418	6,472,661	6,322,259
o/w Rollover	3,777,112	4,615,670	4,948,229	4,028,593	3,990,300	3,990,300
CFS Others	405,954	405,954	435,633	466,128	498,757	533,670
Employee's Contr. To Pension Funds	1,141,144	1,141,144	1,195,882	1,255,676	1,318,460	1,384,383
Recurrent Exp (excl. CFS)	9,719,100	8,354,618	10,250,961	10,522,380	12,163,095	13,432,492
Wages & Salaries	6,600,000	6,367,147	7,205,768	7,627,710	8,999,579	10,110,198
Special Expenditure	305,747	305,747	200,000	200,000	200,000	200,000
LGAs Own Sources	266,166	204,687	274,922	381,443	419,588	461,546
Other Charges	2,547,188	1,477,037	2,570,270	2,313,226	2,543,929	2,660,748
<b>DEVELOPMENT EXPENDITURE</b>	11,820,503	6,498,304	11,999,592	12,248,333	12,129,103	14,333,886
Local	8,702,697	5,141,451	8,969,747	9,536,152	9,409,359	11,565,717
o/w Fuel Levy and Transit Fee	832,349	744,100	917,550	1,194,336	917,550	1,194,336
o/w Railways & Water Fund	287,388	328,772	377,067	433,627	377,067	433,627
o/w Local Govt own source	399,249	307,031	412,384	508,591	412,384	508,591
o/w REA	321,594	334,055	394,952	466,044	394,952	466,044
o/w HESLB	427,555	427,555	427,554	427,554	427,554	427,554
o/w Ports Expansion	510,677	510,677	557,684	607,876	662,585	722,217
o/w TEA	10,000	10,000	10,000	15,000	15,000	15,000
o/w Clearance of arrears	630,000	630,000	1,000,000	1,000,000	1,000,000	1,000,000
Foreign	3,117,805	1,356,853	3,029,845	2,712,181	2,719,744	2,768,169

**Jedwali Na. 2.2: Mfumo wa Bajeti kwa Mwaka 2016/17-2020/21 (% ya Pato la Taifa)**

	2016/17 APPROVED BUDGET	2016/17 ACTUAL BUDGET	2017/18 APPROVED BUDGET	2018/19 PROJECTED BUDGET	2019/20 PROJECTED BUDGET	2020/21 PROJECTED BUDGET
<b>I. TOTAL RESOURCES</b>	<b>27.0%</b>	<b>23.8%</b>	<b>26.2%</b>	<b>24.5%</b>	<b>24.1%</b>	<b>23.6%</b>
Domestic Revenue including LGAs own source	16.9%	16.7%	16.5%	16.6%	16.9%	17.1%
Domestic revenue	16.3%	16.2%	16.0%	16.0%	16.3%	16.5%
Tax Revenue (TRA)	13.8%	14.2%	14.2%	14.2%	14.4%	14.7%
o/w Non Tax Revenue	2.5%	2.0%	1.8%	1.8%	1.8%	1.8%
LGAs Own Sources	0.6%	0.5%	0.6%	0.6%	0.6%	0.6%
Programme loan and grants	0.4%	0.3%	0.8%	0.7%	0.7%	0.6%
Project loans and grants	2.5%	1.9%	2.0%	1.6%	1.5%	1.3%
Basket Support Loans	0.2%	0.1%	0.3%	0.3%	0.2%	0.2%
Basket Support Grants	0.2%	0.2%	0.2%	0.2%	0.1%	0.1%
Domestic Borrowing (Rollover)	3.5%	4.6%	4.1%	3.0%	2.7%	2.4%
Bank Borrowing	1.5%	-0.1%	1.0%	1.0%	1.0%	1.0%
Adjustment to cash	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Non-Concessional borrowing	1.9%	1.2%	1.3%	1.0%	0.9%	0.9%
Financing Gap	0.0%	-1.2%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
<b>II. TOTAL EXPENDITURE</b>	<b>27.0%</b>	<b>23.8%</b>	<b>26.2%</b>	<b>24.5%</b>	<b>24.1%</b>	<b>23.6%</b>
<b>RECURRENT EXPENDITURE</b>	<b>16.2%</b>	<b>17.2%</b>	<b>16.3%</b>	<b>15.2%</b>	<b>15.8%</b>	<b>15.0%</b>
CFS	7.3%	8.8%	7.8%	7.3%	7.6%	6.8%
o/w Interest payments	1.6%	1.7%	1.4%	1.7%	1.9%	1.9%
Pension Bond	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Amortization	4.3%	5.6%	5.1%	4.4%	4.4%	3.8%
o/w Rollover	3.5%	4.6%	4.1%	3.0%	2.7%	2.4%
CFS Others	0.4%	0.4%	0.4%	0.4%	0.3%	0.3%
Employee's Contr. To Pension Funds	1.0%	1.1%	1.0%	0.9%	0.9%	0.8%
Recurrent Exp (excl. CFS)	8.9%	8.4%	8.5%	7.9%	8.3%	8.1%
Wages & Salaries	6.0%	6.4%	6.0%	5.7%	6.1%	6.1%
Special Expenditure	0.3%	0.3%	0.2%	0.2%	0.1%	0.1%
LGAs Own Sources	0.2%	0.2%	0.2%	0.3%	0.3%	0.3%
Other Charges	2.3%	1.5%	2.1%	1.7%	1.7%	1.6%
<b>DEVELOPMENT EXPENDITURE</b>	<b>10.8%</b>	<b>6.5%</b>	<b>9.9%</b>	<b>9.2%</b>	<b>8.2%</b>	<b>8.7%</b>
Local	8.0%	5.2%	7.4%	7.2%	6.4%	7.0%
o/w Fuel Levy and Transit Fee	0.8%	0.7%	0.8%	0.9%	0.6%	0.7%
o/w Railways & Water Fund	0.3%	0.3%	0.3%	0.3%	0.3%	0.3%
o/w Local Govt own source	0.4%	0.3%	0.3%	0.4%	0.3%	0.3%
o/w REA	0.3%	0.3%	0.3%	0.4%	0.3%	0.3%
o/w HESLB	0.4%	0.4%	0.4%	0.3%	0.3%	0.3%
o/w Ports Expansion	0.5%	0.5%	0.5%	0.5%	0.4%	0.4%
o/w TEA	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
o/w Clearance of arrears	0.6%	0.6%	0.8%	0.8%	0.7%	0.6%
<b>Foreign</b>	<b>2.9%</b>	<b>1.4%</b>	<b>2.5%</b>	<b>2.0%</b>	<b>1.8%</b>	<b>1.7%</b>

**Jedwali Na. 2.3: Mfumo wa Bajeti kwa Mwaka 2016/17-2020/21 (% ya Bajeti Yote)**

	2016/17 APPROVED BUDGET	2016/17 ACTUAL BUDGET	2017/18 APPROVED BUDGET	2018/19 PROJECTED BUDGET	2019/20 PROJECTED BUDGET	2020/21 PROJECTED BUDGET
<b>I. TOTAL RESOURCES</b>	<b>100.0%</b>	<b>100.0%</b>	<b>100.0%</b>	<b>100.0%</b>	<b>100.0%</b>	<b>100.0%</b>
Domestic Revenue including LGAs own source	62.5%	70.4%	63.0%	68.0%	70.2%	72.3%
Domestic revenue	60.3%	68.2%	60.8%	65.4%	67.6%	69.7%
Tax Revenue (TRA)	51.1%	59.8%	53.9%	57.9%	60.0%	62.0%
o/w Non Tax Revenue	9.1%	8.5%	6.9%	7.5%	7.6%	7.6%
LGAs Own Sources	2.3%	2.2%	2.2%	2.6%	2.6%	2.6%
Programme loan and grants	1.6%	1.5%	3.0%	2.9%	2.7%	2.5%
Project loans and grants	9.3%	7.9%	7.8%	6.6%	6.1%	5.6%
Basket Support Loans	0.7%	0.4%	1.1%	1.1%	1.0%	0.9%
Basket Support Grants	0.6%	0.7%	0.6%	0.6%	0.6%	0.5%
Domestic Borrowing (Rollover)	12.8%	19.5%	15.6%	12.4%	11.3%	10.2%
Net Domestic Financing	5.4%	-0.5%	3.8%	4.1%	4.2%	4.2%
Adjustment to cash	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Non-Concessional borrowing	7.1%	5.2%	5.0%	4.2%	3.9%	3.6%
Financing Gap	0.0%	-5.1%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
<b>II. TOTAL EXPENDITURE</b>	<b>100.0%</b>	<b>100.0%</b>	<b>100.0%</b>	<b>100.0%</b>	<b>100.0%</b>	<b>100.0%</b>
RECURRENT EXPENDITURE	60.0%	72.5%	62.2%	62.3%	65.8%	63.3%
CFS	27.1%	37.2%	29.8%	29.9%	31.4%	28.9%
o/w Interest payments	5.8%	7.3%	5.4%	6.8%	8.0%	7.8%
Pension Bond	0.0%	0.0%	0.2%	0.0%	0.0%	0.0%
Amortization	16.1%	23.4%	19.3%	17.8%	18.3%	16.2%
o/w Rollover	12.8%	19.5%	15.6%	12.4%	11.3%	10.2%
CFS Others	1.4%	1.7%	1.4%	1.4%	1.4%	1.4%
Employee's Contr. To Pension Funds	3.9%	4.8%	3.8%	3.9%	3.7%	3.5%
Recurrent Exp (excl. CFS)	32.9%	35.3%	32.3%	32.4%	34.3%	34.4%
Wages & Salaries	22.3%	26.9%	22.7%	23.5%	25.4%	25.9%
Special Expenditure	1.0%	1.3%	0.6%	0.6%	0.6%	0.5%
LGAs Own Sources	0.9%	0.9%	0.9%	1.2%	1.2%	1.2%
Other Charges	8.6%	6.2%	8.1%	7.1%	7.2%	6.8%
DEVELOPMENT EXPENDITURE	40.0%	27.5%	37.8%	37.7%	34.2%	36.7%
Local	29.5%	21.8%	28.3%	29.4%	26.6%	29.6%
o/w Fuel Levy and Transit Fee	2.8%	3.1%	2.9%	3.7%	2.6%	3.1%
o/w Railways & Water Fund	1.0%	1.4%	1.2%	1.3%	1.1%	1.1%
o/w Local Govt own source	1.4%	1.3%	1.3%	1.6%	1.2%	1.3%
o/w REA	1.1%	1.4%	1.2%	1.4%	1.1%	1.2%
o/w HESLB	1.4%	1.8%	1.3%	1.3%	1.2%	1.1%
o/w Ports Expansion	1.7%	2.2%	1.8%	1.9%	1.9%	1.8%
o/w TEA	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
o/w Clearance of arrears	2.1%	2.7%	3.2%	3.1%	2.8%	2.6%
Foreign	10.6%	5.7%	9.6%	8.4%	7.7%	7.1%

## 2.3 Vigezo vya Ugawaji Rasilimali fedha katika Kipindi cha Muda wa Kati

77. Katika mwaka 2017/18, Serikali iliandaa kanuni za ugawaji wa rasilimali fedha kwa Wizara, Mkoa, Idara na Taasisi za Umma. Aidha, kwa upande wa Serikali za Mitaa kanuni za ugawaji wa rasilimali fedha zilianza kutumika tangu mwaka 2005/06. Serikali itaendelea kutumia kanuni za ugawaji rasilimali fedha kwa kila fungu kulingana na vigezo vilivyowekwa. Maeneo ya vipaumbele yamebainishwa katika sehemu ya kwanza ya Mwongozo. Aidha, ugawaji wa rasilimali fedha unalenga kuhakikisha miradi/shughuli zinazoendelea zinatengewa fedha pamoja na maeneo mengine muhimu yaliyobainishwa. Mkakati wa ugawaji rasilimali fedha umezingatia kiwango cha asilimia 30 hadi 40 ya bajeti ya serikali katika shughuli za maendeleo.

### 2.3.1 Matumizi ya Kawaida

78. Ugawaji wa rasilimali katika matumizi ya kawaida utazingatia vigezo vifuatavyo:-

- (i) **Mishahara:** Viwango vya mishahara kwa watumishi, idadi ya watumishi waliopo, ajira mpya, nyongeza ya mwaka ya mishahara, upandishwaji vyeo;
- (ii) **Huduma za Mfuko Mkuu wa Hazina:** Makadirio ya gharama kwa ajili ya Deni la Taifa (Mtaji na Riba), michango ya mifuko ya jamii, kiinua mgongo na mafaa ya wastaafu;
- (iii) **Mfuko wa Dharura:** Kanuni ya 22 ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 inaelekeza kutenga asilimia moja ya bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha husika kwa ajili ya mfuko huo;
- (iv) **Matumizi Yaliyolindwa:** Makadirio ya matumizi ya kugharamia uendeshaji wa shughuli muhimu za Serikali. Matumizi hayo ni pamoja na posho ya chakula kwa askari, gharama za kuendesha mitihani kwa shule za msingi na sekondari, posho na mishahara kwa watumishi wanaofanya kazi katika balozi, ruzuku kwa vyama vya siasa, michango ya Serikali kikanda na kimataifa, gharama za pango kwa ofisi za Serikali, stahili za viongozi wastaafu, posho ya mafunzo kwa vitendo, huduma za madawa hospitalini, posho maalum za matabibu, chakula cha wafungwa, na posho ya Jimbo;
- (v) **Matumizi Yasiyojirudia:** Makadirio yanayohusika na shughuli kama Uchaguzi Mkuu, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, sensa ya watu na makazi, n.k.; na
